# Nipashe

Alhamisi Aprili 16, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580207

www.ippmedia.com

The Guardian digital · nipasheTZ · nipasheTZ · nipasheTZ · 0745 700710

LIKE & FOLLOW US




## Watuhumiwa mauaji wauawa wakijaribu kutoroka gerezani

UKURASA 3




UKURASA 11

# Ajali yaua 20, wanne ni ndugu



• **Yumo** bwana harusi mtarajiwa, JPM atuma rambirambi, mfiwa asimulia...

*Endelea ukurasa 2*



Mabaki ya magari mawili, lori lenye namba za usajili T865DQJ Scania lenye tela namba T889DQJ na Coaster Mitsubishi Rosa T102 DSW, baada ya kugongana uso kwa uso katika eneo la Kilimahewa Kaskazini, wilayani Mkuranga, mkoani Pwani jana, na kusababisha watu 20 kufariki dunia na wengine 18 kujeruhiwa. **PICHA: FUTUNA SULEIMAN**



## BAA LA CORONA

**Jeshi la Polisi nchini Kenya, limeanza rasmi kukagua utekelezaji wa amri ya kuvaa barakoa mitaani kama njia ya kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona. Limesema atakayepatikana bila barakoa atatozwa faini Sh. 20,000 au kifungo miezi sita au vyote.**

- **Epuka mikusanyiko ya watu**
- **Nawa mikono kwa sabuni na maji yanayotiririka**
- **Epuka kusalimiana kwa kushikana mikono na kukumbatiana**
- **Ukipiga chafya au kukohoa, ziba mdomo**

## 29 wakutwa na corona, mwingine afa Z'bar

UKURASA 2,8

# Vituo 24 Dar vyatengwa kuchukua sampuli corona

UKURASA 2





Scan Hapa

Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu

GET IT ON Google Play · Download on the App Store



MICHEZO **MWAKALEBELA MAMBO MAGUMU** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6

## Mmoja afariki kwa corona Zanzibar

Na Romana Mallya

IDADI ya vifo vya corona imeongezeka na kufikia vinne baada ya Mtanzania mwenye umri wa miaka 63, mkazi wa Kijichi Visiwani Zanzibar, kufariki dunia nyumbani kwake.

Mpaka sasa watu watatu kutoka Tanzania bara na mmoja visiwani Zanzibar, wamepoteza maisha kwa ugonjwa huo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Waziri wa Afya Zanzibar, Hamad Rashid Mohammed, mwanamume huyo alifariki Ijumaa iliyopita na kuzikwa siku hiyo hiyo.

Mohammed alisema hadi jana kulikuwa na ongezeko la wagonjwa wapya sita kati yao mmoja ni mwanamke na mmoja aliyefariki dunia kufanya jumla ya visa kuwa 18.

Alisema kati yao, Watanzania ni watano na mmoja ni raia wa Misri ambaye aliingia nchini juzi.

"Wagonjwa wapya ni mkazi wa Fuoni (37), mkazi wa Pangawe (45), mkazi wa Kwamchina (60), mkazi wa Migombani (48) na raia wa Misri mwenye umri wa miaka 33, ambaye aliingia nchini jana (juzi) akitokea Misri kupitia Dubai kwa Shirika la Ndege la Fly Dubai," alisema.

Alisema wagonjwa wote ambao ni raia wa Tanzania hawana historia ya kusafiri nje ya nchi siku za hivi karibuni.

"Serikali inaendelea kuwasisitizia wananchi kuchukua tahadhari zote za kujikinga na ugonjwa huu zinazotolewa mara kwa mara ikiwamo kunawa mikono kwa maji ya kutiririka na sabuni kuepuka misongamano na kuahirisha safari za nje na ndani ya nchi zisizo za lazima," alisema.

Pia, aliwataka wananchi wenye dalili za homa kali, kukohoa na kupiga chafya wajitokeze kwenda katika vituo vya afya na kupiga simu namba 190.

"Ni vyema mgonjwa mwenye dalili za maradhi haya asijichanganye na wagonjwa au watu wengine tuache tabia ya kujitibu wenyewe kwani kwa kufanya hivyo tutaendelea kueneza maambukizi na vifo," alisema.



Sehemu ya magari 9 yenye maabara zinazotembea zenye vifaa vya kubaini virusi vya ugonjwa wa corona, yaliyotolewa na serikali ya Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya nchi hiyo ya KFW, kwa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC), yakiwa katika makao makuu ya jumuiya hiyo, jijini Arusha jana, kabla ya kukabidhiwa kwa nchi wanachama. **PICHA: DANIEL SABUNI**

## 20 wafa ajalini akiwamo bwana harusi mtarajiwa

Na Waandishi wetu

WATU 20 wamefariki dunia akiwamo bwana harusi mtarajiwa na wengine 18 kujeruhiwa baadhi yao vibaya katika ajali ya gari iliyotokea katika eneo la Kilimahewa Kaskazini, wilayani Mkuranga, mkoani Pwani.

Kati ya waliofariki, 14 wanaotokea kijiji cha Magawa, ambako gari la kwanza lilianza safari kuelekea jijini Dar es Salaam na kugongana uso kwa uso na Scania.

Kamanda wa Polisi mkoa wa Kipolisi Rufiji, Onesmo Lyanga, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo iliyotokea jana majira ya saa 12:55 alfajiri na kuhusisha gari aina ya Scania lenye namba za usajili T865 DQJ likiwa na tela T 889 DQJ, lililokuwa likitokea Dar es Salaam likiwa na baadhi ya abiria waliokuwa wakielekea kazini Kiwanda cha Tarazo cha Goodwill Ceramic, kilichopo Mkiu Mkuranga.

Liligongana uso kwa uso na gari aina ya Coasta lenye namba za usajili T 102 DSW lililokuwa likitokea Kijiji cha Magawa na Msonga kwenda jijini humo na dereva alifariki papo hapo huku idadi ya abiria wa Scania haijajulikana.

"Kwa ujumla majeruhi 15 waliokolewa walipofika hospitali waliendelea kupoteza maisha na kufikia 20," alisema.

Mganga Mkuu wa Wilaya ya Mkuranga, Dk. Steven Mwandambo, aliwataja waliojeruhiwa na kupelekwa Hospitali ya Taifa Muhimbili (MNH) ni Hija Sakulo, Seif Malwambo, Hamis Matimbwa (32), Ananias Edward (30), Fatuma Athuman, Hamida Athman na Shadia Ali Mbonde.

Wanaoendelea na matibabu Hospitali ya Wilaya Mkuranga ni Abdallah Kassimu (20), Fikiri Miringi (35), Ashraf Rajab (10), Sharifa Said (32), Jaffari Juma (25), Fatuma Mohammed (32) na Maiko Ngaliku (25).

Alisema majeruhi saba waliopelekwa Muhimbili wana majeraha makubwa ambao ni wanaume watano na wanawake wawili.

Kamanda alisema waliokimbizwa Hospitali ya Wilaya ya Mkuranga ni saba miongoni mwao wanawake ni sita na mwanaume mmoja.

"Wanne wapo Kituo cha Afya cha Kilimahewa na miongoni mwao watatu ni wanaume na mmoja ni mwanamke. Waliofariki wanaume ni 12, wanawake ni wanne na mtoto ni mmoja."

Alisema kati ya waliokufa watatu tayari wameshatambuliwa na miili yao imeshachukuliwa na ndugu zao.

Aliwataja waliofariki kuwa ni Fatuma Habibu Mpili (36) Hamis Said Mpili (50) na mfanyakazi wa Goodwill Ceramic, Hemed Said (28).

### ALIYEPOTEZA WANNE ANENA

Akizungumza na Nipashe, Mwandishi wa Habari, Athumani Mtulya, aliyepoteza wanafamilia wanne katika ajali hiyo, alisema mmoja wanandugu hao ni Hashim Mtulya (26), ambaye alikuwa aoe Jumapili ijayo Aprili 19, mwaka huu.

Alisema kijana huyo ni mtoto wa baba yake mkubwa na maandalizi yote ya harusi yalishafanyika ikiwamo kulipa mahari na kutokana na hali ya Corona ilikuwa ifanyike sherehe ndogo jijini Dar es Salaam, ambayo ingehusisha wanafamilia.

"Nimeshafika Hospitali ya Wilaya Mkurunga ambako miili ya ndugu zetu imehifadhiwa na tumeshaitambua, tunasubiri wakamilishe taratibu zao watukabidhi miili kwa ajili ya maziko, tunazika leo," alisema.

"Kijiji cha Magawa ndiyo nyumbani kwetu, ni umbali wa zaidi ya kilomita 90 hadi Dar es Salaam, na hilo ni gari la kwanza ambalo hutoka kijijini saa 11 alfajiri na saa tano asubuhi wameshafika jijini," alieleza.

### RAIS ATUMA SALAMU

Wakati huo huo, Rais Dk. John Magufuli, ametuma salamu za rambirambi kwa ndugu, jamaa na marafiki wa waliopoteza maisha katika ajali hiyo na kuwaombea waliojeruhiwa wapone haraka na roho za marehemu zipumzike pema peponi.

Kwa mujibu wa taarifa kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Rais amemtaka Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Evarist Ndikilo, kufikisha salamu zake za pole kwa familia za marehemu na ameeleza kwamba anaungana nao katika kipindi hiki cha majonzi ya kuondokewa na wapendwa wao.

"Nawaombea familia za marehemu wote, ndugu, jamaa na marafiki kuwa na moyo wa uvumilivu na ustahimilivu katika kipindi hiki kigumu cha majonzi, kuwapoteza Watanzania wenzetu kwa idadi kubwa namna hii inaumiza sana," alisema Rais Magufuli.

■**Imeandikwa na Salome Kitomari (DAR) na Futuna Seleman, MKURANGA**

## Vituo 24 Dar vyatengwa kuchukua sampuli corona

Na Romana Mallya

VITUO 24 vimetengwa mkoa wa Dar es Salaam kwa ajili ya kuchukua sampuni za washukiwa wa virusi vya corona, lengo likiwa ni kupunguza maambukizi zaidi.

Kwa mujibu wa taarifa ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda jana, vituo hivyo vimetengwa kila wilaya mkoani humo.

Makonda alisema katika Manispaa ya Kinondoni vimetengwa vituo sita ambavyo ni hospitali za Mwananyamala, Magomeni, Rabininsia, TMJ na kituo vya afya cha IST na Mikoroshini.

"Manispaa ya Ilala kutakuwa na vituo saba ambavyo ni hospitali ya Amana, Buguruni, Mnazi Mmoja, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH), Hindu Mandal, Aga Khan na Regency.

Alisema katika Wilaya ya Temeke kutakuwa na vituo vinne ambavyo ni hospitali ya Temeke, Mbagala Rangi Tatu, Yombo na TOHS.

"Halmashauri ya Ubungo kutakuwa na vituo vinne ambavyo ni hospitali ya Sinza, Bochi na Mlongazira na kituo cha afya cha Kimara," alisema.

Makonda alisema katika Halmashauri ya Kigamboni kutakuwa na vituo vitatu ambavyo ni hospitali binafsi ya Aga Khan na kituo cha afya cha Vijibweni na Kigamboni.Alisema wahisiwa wote wa ugonjwa wamekuwa wakipimwa katika Maabara Kuu ya Taifa na majibu yao hupatikana kwa wakati kama muongozo unavyoelekeza.

"Changamoto moja wapo ambayo imekuwa ikijitokeza ni kwa baadhi ya watu wenye dalili kupita katika vituo kadhaa vya kutoa huduma za afya, hivyo kuchangamana, kukutana na watu kadhaa kabla ya kugundulika kuwa ni wagonjwa.

"Hali hii inaweza kuchangia kuongezeka kwa visa vya corona kwa kasi kubwa. Mkoa umejipanga kupunguza ueneaji wa ugonjwa kwa kuainisha vituo maalum vya wahisiwa wanaokidhi vigezo vya tafsiri ya ugonjwa kuchukuliwa sampuli.

"Ieleweke kuwa vituo hivi havitatumika kupima sampuli bali ni vya kukusanya sampuli za wahusika tu." Alisema vituo hivyo vitawawezesha wahusika kupata huduma ya vipimo kwa kuchukuliwa sampuli katika maeneo yao ya karibu kabla ya kuchangamana na watu wengine kwa sababisha kusambaza virusi hivyo.

Alisema vituo hivyo vitaongeza kasi ya mapambano dhidi ya ugonjwa huo.

# Mapendekezo manane ya ACT kuhami uchumi

**Na Maulid Mmbaga**

CHAMA cha ACT-Wazalendo, kimependekeza mambo manane ya kuhami Uchumi wa nchi na kuukabiliana na corona.

Katika taarifa iliyotolewa na chama hicho jana, kupitia Katibu Mkuu wa chama hicho, Ado Shahidi na Naibu Katibu Mkuu wa chama hicho Zanzibar, Nassor Mazrui, walisema ugonjwa huo umeathiri sekta mbalimbali za kibiashara nchini zikiwamo za kiserekali na binafsi.

Aidha, walipendekeza majiji ya Mwanza, Arusha, Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar kufungwa siku 30.

Chama hicho kilipendekeza kuwa watumishi wa umma katika mikoa husika wafanyie kazi majumbani mwao kwa kuwa vipato vyao ni vya uhakika, na kwamba ofisi za umma zibakize mtu mmoja kwa idara na kwa zile kazi ambazo hazihusishi kukutana na watu na iwe kwa zamu.

Walisema ofisi za umma za kutoa huduma kwa wananchi kama vituo vya huduma za afya na polisi waendelee na kazi kwa kupewa vifaa maalumu vya kuzuia maambukizi ya virusi vya COVID 19.

Walisema kumbi za starehe, shughuli za michezo na maeneo ya vinywaji kama vile baa na vilabu vya pombe visimame, pamoja na watoa huduma za vyakula kama mamalishe waendelee na shughuli zao kwa uangalifu mkubwa na inapobidi watumike kusambaza vyakula majumbani kwa watu watakaohitaji msaada.

Aidha, masoko ya mazao yawe wazi kwa usimamizi maalum wa uongozi wa soko na mamlaka za Serikali za Mitaa kuweka utaratibu maalumu wa wananchi kuhemea, masoko ambayo hayatafuata maagizo yafungwe bila kuchelewa.

Pia, vyombo vya usafiri viendelee kwa maelekezo maalumu ya kuhakikisha kuwa hakuna msongamano kwenye viti, na magari ya jeshi yatumike kupakia abiria kuondoa msongamano.

Lingine ni kupunguza msongamano magerezani kwa kuwapa dhamana watu wanaostahili, kuwapa dhamana watu wote ambao kesi zao upelelezi unaendelea, kuwaachia huru watu wote wenye umri unaozidi miaka 65, wanawake wenye watoto kwa ujumla. Walisema hospitali binafsi zenye uwezo kuwa sehemu ya karantini na (isolation) kuepusha kuelemewa kwa vituo vya umma vilivyopo sasa.

"Wako watu wenye uwezo wako tayari kulipia kukaa hospitali wanazozipenda wao wakiugua corona," ilieleza taarifa. Kuhusu wasio na ajira, ACT-Wazalendo inapendekeza walipwe na mifuko ya Hifadhi ya Jamii Fao la upotevu wa ajira, ili kuweza kuendelea na maisha, na kila kaya kupewa kiasi cha Sh. 300,00 kila mwezi.

**Lingine ni kupunguza msongamano magerezani kwa kuwapa dhamana watu wanaostahili, kuwapa dhamana watu wote ambao kesi zao upelelezi unaendelea, kuwaachia huru watu wote wenye umri unaozidi miaka 65.**

## Watuhumiwa mauaji wauawa wakijaribu kutoroka gerezani

**Na Neema Emmanuel, MWANZA**

WATUHUMIWA wawili wa kesi za mauaji na mfungwa mmoja wamefariki dunia nyakati tofauti walipojaribu kutoroka katika Gereza Kuu la Butimba mkoani Mwanza.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Mwanza, Muliro Jumanne, alisema April 14, mwaka huu majira ya alfajiri eneo la Gereza Kuu Butimba, watuhumiwa watatu ni Yusuph Benard (34), ambaye ni mahabusi namba 3444/2016, Seleman Seif ( 28), mahabusi namba 1177/2017 na George Aloyce(34), mfungwa no 200/2019 walijaribu kutoroka ndipo askari Magereza wakishirikiana na wananchi waliwakimbiza na kufanikiwa kuwakamata.

Alisema baada ya kukamatwa, wananchi waliwashambulia kwa kipigo katika sehemu mbalimbali za miili yao, na kwamba waliamua kuwapeleka Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Mwanza Sekou Toure kwa ajili ya matibabu, lakini majira ya saa 18:30 jioni walifariki dunia wakati wakiendelea na matibabu.

Aliongeza kuwa mtuhumiwa wa tatu, George Aloyce, aliyekuwa amefungwa kwa miaka 15 kwa kosa la uhujumu uchumi, huku akiwa na kifungo kingine cha miezi sita, alijaribu kutoroka tena katika Gereza la Butimba, baada ya kukamatwa na kuhojiwa na polisi, aliwaeleza kuwa endapo wangefanikiwa kutoroka wangechukua teksi eneo la Mabatini Wilaya ya Nyamagana .

" Baada ya kupata maelezo hayo, Polisi walimtaka hawapeleke ili kuwaonyesha huyo dereva teksi ambaye angewasafirisha kuwapeleka eneo la Katoro mkoani Geita, lakini walivyoshuka kutoka kwenye gari na kuanza kutembea huku akijidai anataka kuwaonesha muhusika, ghafla alianza kukimbia ndipo askari polisi waliokua nae walimwamuru kusimama huku wakipiga risasi juu," alisema Muliro na kuongeza:

"Kakini hakutii amri ndipo walimrushia risasi zilizomjeruhi miguuni na kufanikiwa kumkamata na kumpeleka Hospitali ya Rufani ya mkoani hapa Sekou Toure ambapo baadae naye alifariki."




# PM aamuru mfanyabiashara achukuliwe hatua

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa, ameiagiza Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa (KUU) wa Mwanza, imchukulie hatua za kisheria mfanyabiashara aliyekamatwa kwa makosa ya kujihusisha na biashara ya zana haramu za uvuvi.

"Yuko mfanyabiashara anaitwa Jeremiah Asam Omolo, amekamatwa mara kadhaa kwa kukutwa na nyavu haramu. Wizara ilitoa specifications (aina ya nyavu) zinazoruhusiwa kutumika na KUU ya Mkoa ikasimamia, lakini kuna maofisa wa wizara waliingilia zoezi hilo mara tatu na akatozwa faini mara zote," alisema.

Waziri Mkuu alitoa agizo hilo jana, wakati akizungumza na Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa wa Mwanza, kwenye kikao alichokifanya kwa njia ya video (video conference) kutokea ofisini kwake Mlimwa, jijini Dodoma.

"Mkuu wa Mkoa aliunda timu ya kuchunguza matukio haya. Hii ni timu ya serikali na imeaminiwa kufanya kazi hii, na ina uwezo wa kuchukua hatua. Lazima KUU ya mkoa isimamie na ichukue hatua. Hatuwezi kuwa na Wizara ambayo haiamini KUU ya mkoa," alisisitiza.

Alisema hatua pekee zilizochukuliwa na wizara ni kumtoza faini mfayabiashara huyo kwa kumlipisha zaidi ya Sh. milioni 470. "Lengo la serikali siyo kutoza fedha peke yake, bali ni kudhibiti matumizi ya nyavu haramu nchini," alisisitiza.

Alisema kwa kuwa si mara yake ya kwanza kukamatwa, KUU ya Mkoa haina budi kuchukua hatua kali zaidi kwa sababu nia ya kutoa adhabu ni kumfanya mkosaji asirudie kosa, lakini mfanyabiashara huyo amekuwa akilipa faini na kurudia makosa yaleyale.

Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, John Mongella alisema, katika kosa la kwanza, mfanyabiashara huyo alipatikana na marobota 66 ya nyavu haramu aina ya makila sawa na vipande 13,200 na alitozwa faini ya Sh. milioni 50.

Alisema katika tukio la pili, Aprili 3, mwaka huu, Omolo alikutwa na zana haramu za uvuvi aina ya makila vipande 6,964 na Timba vipande 179 na kutozwa faini ya Sh. milioni 129.8.

"Katika tukio la tatu, Aprili 4, 2020 alipatikana na kosa la kumiliki zana haramu za uvuvi ambazo ni marobota 10 ya nyavu haramu aina ya makila sawa na vipande 300 na marobota 437 ya nyavu haramu aina ya Timba sawa na vipande 12,875 na kutozwa faini ya Sh. milioni 300," alisema.

Alisema uongozi wa mkoa uliamua kuunda timu ya wataalamu inayojumuisha vyombo vya usalama ambavyo itafuatilia na kuchunguza kwa undani mienendo ya mtuhumiwa huyo ikiwamo suala la kikodi na ufanyaji wa biashara.

Alimwambia Waziri Mkuu kwamba timu hiyo iliyoundwa Aprili 9, mwaka huu, itapaswa kukamilisha kazi yake na kukabidhi taarifa yake, Jumatatu ijayo (Aprili 20, 2020).

Wakati huohuo, Waziri Mkuu amekemea mikusanyiko inayofanyika kwenye nyumba za ibada kwa kigezo cha kutaka watoto wasikae majumbani kwa vile hawaendi shuleni.

"Ninazo taarifa kwamba wameanzisha mfumo wa kupeleka watoto kwenye madarasa ya dini maarufu kama Sunday School. Tumeruhusu ibada tu, na hizo ibada lazima ziangaliwe ziwe za muda mfupi kadri inavyowezekana. Tumesisitiza kwenye makanisa au misikiti ambako ibada zinafanyika, waumini wakae kwa kuachiana nafasi."

Amesema changamoto inajitokeza kwenye makanisa makubwa ambayo yana waumini karibu 3,000. "Hayo sasa yatakuwa ni makongamano. Tunaamini maaskofu na Mufti wataliweka vizuri suala hili la Sunday school na madrasa," alisema.



Mkurugenzi wa TBL Plc, Philip Redman (wa nne kulia), akimkabidhi msaada wa tani 9 za unga wa mahindi kwa Mbunge wa jimbo la Rufiji mkoa wa Pwani, Mohamed Mchengerwa, zilizotolewa na kampuni hiyo, jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya wahanga wa mafuriko yaliyotokea hivi karibuni, wilayani Rufiji. Wengine ni wafanyakazi wa kampuni hiyo.

# Bila barakoa huingii KCMC

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

HOFU ya kuongezeka zaidi idadi ya watu wanaougua homa ya kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona, imesababisha Hospitali ya Rufani ya Kanda KCMC, kuweka sharti gumu kwa watu wanaoingia katika lango kuu la hospitali hiyo kuvaa barakoa.

Uamuzi huo unalenga kukabiliana na kasi ya maambukizi ya Covid - 19.

Jana, Ofisa Uhusiano wa KCMC, Gabriel Chisseo, alisema tahadhari hiyo imechukuliwa ili kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo kusambaa.

"Ni kweli hata wazee hawaruhusiwi tena kwenda kuchukua dawa, badala yake wanapaswa kutuma watoto wao au walezi kuwachukulia dawa.

"Pia tumechukua tahadhari nyingine ya kupunguza idadi ya wanafamilia wanaokwenda kuhudumia wagonjwa kuwa mmoja, na kuingia KCMC tumesema ni lazima uvae barakoa."

## CAG abaini tatizo TBS

**Na Mwandishi Wetu**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu (CAG), amebaini dosari katika utekelezaji wa majukumu ya kisheria ya Shirika la Viwango (TBS).

Katika ripoti yake ya ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/19, CAG Charles Kichere, anasema TBS ilianzishwa ili kukuza viwango na uhakiki wa ubora katika viwanda na biashara nchini.

Anasema amepitia utendaji wa shirika ili kufahamu iwapo linafanya kazi zake kwa mujibu wa sheria iliyolianzisha na amebaini dosari katika upakuaji wa kontena bila kushuhudiwa na mawakala na kuweka muhuri wa 'Tamper-proof'.

Anasema kipengele cha 2.3.2 (l) cha Mahitaji Maalum ya Masharti ya jumla ya mkataba kati ya TBS na wakala aitwaye Bureau Vetaris; Intertek International; na SGS kinataka wakala kushuhudia upakuaji na uwekaji wa muhuri kwenye makontena.

"Mapitio ya mkataba kati ya TBS na mawakala wa PVoC ilioingia (assigned in) jijini Instabul, Uturuki na Dubai (United Arab Emirates), yalibaini kuwa mawakala wawili kati ya watatu hawakushuhudia upakuaji na uwekaji wa muhuri kwenye kontena kwa mizigo yote iliyoletwa Tanzania Bara kati ya Septemba Mosi, 2018 na Juni 30, 2019.

"Wakala mmoja ndiye alishuhudia kontena lililopakua bidhaa zenye hatari ambazo walizionyesha kwa uzoefu. Nilipowauliza mawakala, walinieleza kuwa kipengele cha 2.3.2 (l) ni kipana sana, hivyo wanasubiria maelekezo ya shirika kuhusu namna ambavyo upakuaji na uwekaji wa mihuri kwenye kontena unatakiwa ufanyike kwa sababu hauwezi kufanyika kwa mizigo yote inayoletwa. "Maelekezo yanatakiwa kuonyesha orodha ya bidhaa zenye hatari ambazo uhakiki wa lazima wakati wa upakuaji unatakiwa kufanyika. Mfano, kuna gharama zinazoambatana na uhakiki wa upakuaji wa kontena na changamoto za mizigo inayopakiwa mmoja mmoja (Loose Cargo Loads) na mizigo inayofungwa kwa pamoja (Full Cargo Loads).

"Shirika la Viwango Tanzania, lilitakiwa kuona mbali kwa kuandaa na kuwashirikisha mawakala maelekezo yaliyopo kwenye mkataba uliosainiwa. Mizigo isiyoshuhudiwa inaacha upenyo wa kuingiza bidhaa zisizokuwa na viwango.

"Shirika lilieleza kuwa, orodha ya bidhaa zenye hatari tayari ipo kwa ajili ya mazungumzo na makubaliano ya mwisho na watoahuduma kwenye kikao cha pamoja ambacho kilipangwa kifanyike mwezi Februari 2020," anasema.

CAG anapendekeza shirika liandae na kushirikisha maelekezo ya mkataba kwa mawakala baada ya kufanya tathmini ya hatari kwa bidhaa zote zinazoingizwa na kuzigawa bidhaa kulingana na kiwango cha hatari na kufanya uamuzi bidhaa zipi zitafanyiwa uhakiki wa lazima.

Pia, anapendekeza shirika liwasiliane na mawakala wa PVoC na kukubaliana njia inayofaa ya kutekeleza mkataba.

TANGAZO


MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA

Imethibitishwa na ISO 9001: 2015

# HUDUMA ZA TRA KWA NJIA YA MTANDAO

**Ndugu mlipakodi TRA inakukumbusha kuwa, huduma zifuatazo zinapatikana kwa njia ya mtandao bila kulazimika kufika ofisini;-**

1. Usajili wa TIN unaotumia namba ya kitambulisho cha taifa,
2. Makadirio na malipo ya kodi ya majengo,
3. Kujisajili kwa ajili ya kufanya malipo ya kodi moja kwa moja kupitia mfumo wa Revenue Gateway System na GePG,
4. Kuwasilisha kadhia za forodha kupitia mfumo wa TANCIS,
5. Kikokotoo cha magari yaliyotumika na kununuliwa kutoka nje ya nchi,
6. Kikokotoo cha kodi za ajira,
7. Minada kwa njia ya mtandao,
8. Maulizo na uwasilishaji malalamiko katika kituo cha huduma,
9. Kuchapisha cheti cha kodi ya zuio,
10. Uwasilishaji wa ritani za kodi ya ongezeko la thamani (VAT).

**Kumbuka kuwa, unaweza kupata fomu mbalimbali kwa kutembelea tovuti yetu ya www.tra.go.tz**

**Kwa mawasiliano zaidi tufikie kwa kutumia mawasiliano yafuatayo;-**

**Simu za bure: 0800-750075 au 0800-780078**

**WhatsApp: 0744-233 333**

**Barua pepe: huduma@tra.go.tz**

***"Pamoja Tunajenga Taifa Letu"***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni muhimu kwa kila mtu kuvaa barakoa

**HIVI** karibuni Serikali ilitangaza kuwa janga la corona limeingia kwenye jamii na sasa wanaoambukizwa inakuwa ngumu kujua walikopatia maambukizi hayo.

Kutokana na hali hiyo, tayari zaidi ya Watanzania 88 wameabukizwa kwa maambukizi ya ndani hadi jana jioni, ikiwa na maana kwamba wapo watakaoambukizana bila kujua hadi dalili zitakapojitokeza wazi.

Kutokana na janga hili, Serikali imepokea fedha taslimu na vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni 6.7, kutoka kwa wadau mbalimbali kwa ajili ya kupambana na corona.

Juzi, Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Richard Kasesela, alielekeza wamiliki wa baa kuhakikisha wahudumu wao wanavaa barakoa, ikiwamo kuhakikisha kuna maji yanayotiririka na sabuni.

Aidha, Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), lilieleza kuwa kuna utafiti wa awali umeonyesha kuwa, huenda virusi hivyo vinaweza kuambukizwa kwa hewa kwa kuwa vina uwezo wa kukaa kwenye hewa kwa saa kadhaa. Kutokana na hali hiyo, Waziri alieleza anaona kuna umuhimu wa watu kuvaa barakoa ili kujikinga zaidi, ikiwamo kutoambukiza watu wengine.

Tunaona ni muhimu suala la kuvaa barakoa likatiliwa maanani kwa kila mtu anayekuwa kwenye msongamano, ikiwamo kwa wafanyakazi wa kampuni husika kuhakikisha watumishi wake wana vifaa hivyo. Maeneo ambayo tunaona watu wanatakiwa kuvaa barakoa ni kila anayekwenda kituo cha afya, zahanati na hospitali yoyote nchini kutoruhusiwa kuingia kabla ya kuvaa barakoa.

Tumeona tayari hospitali ya Rufani ya KCMC imebandika tangazo kwamba hakuna atakayeruhusiwa kuingia hospitalini humo bila kuvaa barakoa, jambo ambalo ni zuri na linapaswa kuingwa na hospitali zingine.

Maeneo mengine ni kwenye vituo vikuu na vidogo vya mabasi kwa maana ya wasafiri, makondakta, madereva na wapigadebe kuhakikisha wamevaa vifaa hivyo, ili kuepuka kuambukizana.

Maeneo mengine ni kwa mama lishe ambao hupokea watu wengi wenye hulka tofauti, ambao wao wenyewe wanapaswa kujikinga na wateja wao, ikiwamo kuweka mgomo kutouza chakula kwa mtu ambae hajajikinga wakati wa kuagiza.

Wengine ni wenye maduka ya vyakula ambao hupokea watu wengi kwa kutwa wanaokwenda kununua bidhaa. Tunatambua kuwa kila anayefika anatakiwa kunawa mikono, lakini hiyo pekee haitoshi kwa kuwa bado upo uwezekano wa mtu kupiga chafya au kukohoa na wadudu kutoka na kusambaa kwenye hewa.

Maeneo mengine ni kwenye masoko ambako kuna mikusanyiko ya watu wengi, nako tunaona ni muhimu wakavaa barakoa kwa maana kuna wateja na wauzaji, hivyo kuwa rahisi kuambukizana ugonjwa huo kwenye jamii.


Eneo jingine ambalo ni hatarishi ni Soko la Kariakoo jijini Dar es salaam, ambako hukusanya idadi kubwa ya watu ambao hununua na kuuza bidhaa zao, hivyo ni muhimu kila mmoja akavaa barakoa ili kuepusha kusambaza ugonjwa huo iwapo mmojawapo atakuwa nao.

Pia, ni vyema viongozi wa dini wakawasihi waumini wao kuanza kuvaa barakoa ili kuwa salama zaidi kwa kuwa picha ya utaratibu mpya wa sasa wa waumini kukaa mbalimbali, ni nzuri, lakini bado ipo hatari.

Hatari ni kuwa katika ibada waumini huimba au kufanya kiitikio, kwa hiyo upo uwezekano wa mtu kutokwa na mate bila kujijua na kusambaa na kwenda kwa mti aliyeko mbele au pembeni yake, na kama virusi vinaweza kuishi kwenye hewa kwa saa tatu, maana yake uwezekano wa mwingine kupata ni mkubwa.

Katika kufanikisha hili tunashauri serikali kuweka zuruku kwenye viwanda vinavyotengeneza barakoa, ikiwamo kuzigawanya bure kwa wananchi wa kipato cha chini kwenye mitaa na hasa zile zinazoweza kudumu kwa mwezi mmoja.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



# Kunawa mikono tumefanikiwa, lakini Mabibo Sokoni...mmh!

Na Yasmine Protace

**UNAWAJI** mikono ni sehemu ya faida ya mtu kujikinga na maambukizi ya magonjwa ya kuambukiza, kokote aliko.

Mara nyingi jamii imekuwa ikielimishwa faida za kunawa mikono, wakati wa kutaka kula na hata kumaliza mlo. Mbali na kutaka kula au kumaliza mlo, pia hata mtu anapotoka msalani, iwe haja kubwa au ndogo, unawaji mikono ni suala la lazima.

Kimsingi, mtu anapotoka matembezini au safari zozote, anapofika nyumbani anashauriwa kunawa mikono kwa maji akitumia maji yanayotiririka. Hilo ni agizo la kiafya sasa, kitaifa na kimataifa, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Hivi sasa tuko katika pilika la janga la corona, kumekuwapo nchi nyingi zenye matatizo kwa ngazi tofauti, zipo zilizokumbwa na zingine ziko katika hatua ya kujikinga kuhakikisha hazifikiwi, iwe kitaifa au majimbo na mikoa ya nchi.

Kwa sasa, nikirejea tovuti ya kitaifa ya Worldometer, hadi jana nchini tunahesabiwa waliofikwa na maradhi haya, idadi yao ni 59, vifo vitatu na waliopona wako saba,

Serikali nchini inaendelea kutoa elimu ya kunawa mikono kama hatua ya kwanza, ikifuatiwa na nyinginezo zinazohakikisha wananchi hawafikiwi na virusi hivyo hatari.

Darasa ni pana, kwa walimu inayotolewa kwa njia nyingi kama magazeti, televisheni, redio an viongozi wa kitaifa kuanzia sekta ya afya na nje ya sekta hiyo zikiwamo nyumba za ibada, shule ya kunawa mikono iko juu.

Mengine ni watu wanatakiwa kukwepa mikusanyiko, kutojazana katika vyombo vya moto inahimizwa kwa namna nyingi.

Juzi, serikali katika mwendelezo wa vita hivyo, ilitangaza shule kufungwa hadi pale serikali itakapotangaza tena. Ni ishara ya hatari, kwa maana ya rekodi yetu imefika hatua ya kuchukua uhai wa wenzetu kadhaa.

Katika kupambana, eneo la masoko mengi wamejitahidi kutia maanani yaliyosistizwa. Kumewekwa maji na sabuni, ili waingiaji wanawe mikono mlangoni huko, kabla ya kuingia huko wanakoenda kupata mahitaji na hata wanapotoka.

Mtu anapofika katika maduka mbalimbali, ni kawaida akakuta ndoo za maji na sabuni, ikiwa ni kiashiria kizuri kwamba wananchi wameelimika vyema katika hatua ya kujikinga na corona, hasa kupitia kinga za mwanzo; maji, sabuni na vitakasa mikono.

Ila kuna ninachothubutu kuwaza, kwamba wapo wasio na mwamko katika suala la usafi wa mikono yao, eneo nililodokeza kushuhudia mafanikio makubwa katika sehemu nyingine, ikiwamo sokoni ambako ndiko kuna dhamira ya hoja yangu.

Katika soko la Mabibo jijini Dar es Salaam, eneo la lango la kuingilia sokoni, kuna maji yaliyowekwa na kuna askari mgambo anayeshika kipaza sauti na kuelimisha na kuwahimiza wananchi wanaoingia sokoni, kuhakikisha wananawa mikono yao.

Pamoja na elimu hiyo thabiti kupitia kipaza sauti, nina ushuhuda unaonishangaza kuwaona baadhi ya watu hawana uelewa wanaoambiwa kuhusu dhamira ya kunawa mikono.

Nimewashuhudia wengi wanaingia sokoni Mabibo bila ya kunawa mikono yao, tena katika mwendelezo wa mshangao kutoka ushuhuda binafsi, mtu anatangaziwa elimu umuhimu ya kunawa mikono, anaishia kupuuza.

Kama mtu anakataa kunawa mikono yake, anategemea nini kinamtokea kwa kutonawa mikono? Ni busara tuzingatie maelezo kutoka kwa wataalamu wa kunawa mikono, tuachane na mkusanyiko mkubwa kwa muda na kuendelea kufuata kwa hatua tunayoambiwa na viongozi wetu.

Hata kuna kingine kinachoshangaza, kuna wanaofuatwa kukumbushwa wajibu huo wa kunawa mikono, bado wanagoma na kutii hilo.

## HABARI KITAIFA

### Ujerumani yatoa magari 9 maabara zinazotembea

**Na Daniel Sabuni,**
ARUSHA

SERIKALI ya Ujerumani kupitia Benki ya Maendeleo ya Ujerumani, imetoa msaada wa magari tisa ya maabara zinazotembea kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki yenye thamani ya Dola za Kimarekani milioni 1.8.

Magari hayo yana vifaa vya kupimia virusi vinavyosababisha homa kali mapafu Covid-19 na magonjwa mengine.

Katibu Mkuu wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, Balozi Liberat Mfumukeko, alisema katika mgawo wa maabara hizo Tanzania imepata magari mawili , Kenya mawili, Uganda mawili, Sudani Kusini, Rwanda na Burundi kila moja imepata gari moja.

"Baadhi ya nchi zimepata magari zaidi kuliko nyingine sababu ya wingi wa watu, maana ukiwa na watu wengi unahitaji zaidi ili kuwa na uwiano kupata huduma kwa haraka, malengo yetu kama mtu ameambukizwa apate majibu ya damu yake haraka na kwa kufanya hivyo itasaidia nchi kupanga namna ya kudhibiti," alisema.

Pia kuna magari mengine mawili zaidi kwa nchi za Tanzania, Kenya na Uganda, wakati Sudani Kusini, Rwanda na Burundi zimepata moja zaidi ili kuwezesha wataalamu wa afya watakaotoa huduma kupitia maabara wayatumie kuwafikisha wanapokwenda kuhudumia wananchi.

"Maabara hizi zina kila kinachohitajika kwa huduma kama kupima, kuzuia, nina imani kubwa zitasaidia mapambano ya vita vya virusi vya Covid-19 kwa Jumuiya ya nchi wanachama pamoja kudhibiti magonjwa kama ebola na homa ya manjano," alisema Mfumukeko.

# Serikali yatoa msimamo kung'olewa kwa mameya

**Na Augusta Njoji,**
DODOMA

BUNGE limepitia bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) kwa mwaka 2020/21,Sh. trilioni 7.019, huku serikali ikitaka uamuzi ya baraza la madiwani ya kuwaondoa mameya uheshimiwe.

Akihitimisha hoja ya bajeti hiyo juzi bungeni, Waziri wa Ofisi hiyo, Selemani Jafo, alisema kumekuwapo na hoja kuhusu kuondolewa kwa mameya wa Dar es Salaam na Iringa, na kwamba ni vyema uamuzi huo uheshimiwe.

Alisisitiza kuwa si viongozi hao walioondolewa madarakani, kwani kuna wenyeviti watatu wa halmashauri ambao ni wa Chama cha Mapinduzi(CCM), pia wameondolewa.

Kuhusu hoja ya fedha za maendeleo kutolewa kulingana na ukubwa wa jimbo, Jafo alisema serikali inafanyia kazi hoja hiyo.

Akizungumzia kuhusu kuongezea fedha Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (Tarura), Waziri Jafo alisema Ofisi hiyo ina mikakati ya kutafuta fedha kutoka vyanzo vingine ili kutengeneza barabara kwa ufanisi, na kuwa Tarura ina mtandao mkubwa wa barabara.

"Pamoja na kuja na fomula endelevu ya kugawa fedha za barabara, lakini pia tunamkakati wa kutafuta fedha katika vyanzo vingine kama tulivyofanya katika kuboresha Jiji la Dar es Salaam, kuna miji ambayo pia inaboreshwa na baadaye tutakuja na halmashauri 45 zingine," alisema Jafo.

Kuhusu posho za madiwani, Jafo alisema Ofisi yake itahakikisha hadi kufika Mei 30,mwaka huu madiwani wanalipwa malimbikizo ya posho zao. Akijibu hoja ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwamba kuna Sh. bilioni 184.1 ambazo hazijatolewa kwa ajili ya umaliziaji wa maboma sekta ya afya na elimu, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Ashatu Kijaji, alisema si kweli, kwa kuwa kila mwaka serikali imekuwa ikitenga na kutoa fedha zote.

Alisema kwa mwaka ujao 2020/21, serikali imetenga Sh. bilioni 228.15 na zitatolewa zote kwa ajili ya kukamilisha maboma ya sekta ya afya na elimu.

"Katika bajeti ambayo inaheshimiwa sana ni ile ya kumalizia nguvu ya wananchi... kuanzia mwaka 2017/18 bajeti yote inayotengwa kwa ajili ya maboma imekuwa ikitolewa na mwaka 2017/18 tulipanga Sh. bilioni 38.9 na tulitoa zote kwa ajili ya umaliziaji maboma 96 ya vituo vya afya," alisema.

Aidha, alisema kwa mwaka 2018/19 zilitengwa Sh. bilioni 29.9, kukamilisha maboma 2,392 ya madarasa ya shule za sekondari na zilitolewa zote.

"Mwaka 2019/20 zilipitishwa Sh. bilioni 19.5 na zimetolewa zote hadi sasa kwa ajili ya kukamilisha 364 nyumba za walimu kwenye shule za msingi na maboma ya zahanati 52," alisema.







Mkuu wa Mkoa wa Arusha, Mrisho Gambo (kushoto) na Meneja Mkuu wa kampuni ya Mega Beverages, Chris Ndosi, wakimkabidhi msaada wa lita 200 za vitakasa mikono na ndoo 10 za kunawia mikono Kaimu Kamanda wa Polisi wa mkoa huo, Koka Moita, jijini humo jana, ikiwa ni sehemu ya msaada uliotolewa na kampuni hiyo, ili kupambana na maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa Corona. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Waziri amsweka ndani mkandarasi kisa ajali

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amemsweka ndani mkandarasi wa Kampuni ya Nangonga Building and Cicil Contractors, Mohammed Nangonga, kutokana na kushindwa kuweka alama za barabarani wakati akikarabati mashimo eneo la barabara ya Morogoro-Dodoma, hivyo kusababisha ajali za vifo vya watu watatu.

Simbachawene alisema kuwa eneo la Ihumwa ambako ndiko kulikokuwa kukifanyika ukarabati huo, juzi kulitokea ajali hiyo ambayo ilisababisha vifo vya watu wawili hapo hapo gari lilipokuwa linakwepa shimo ambalo lilikuwapo eneo hilo.

Juzi pia lori lililokuwa limebeba saruji likitoka Dar es Salaam kwenda Kigoma, lilipata ajali ya kugongana na basi, hivyo kusababisha kifo cha utingo wa lori hilo.

Kutokana na ajali hizo, Waziri Simbachawene alifika katika eneo la ajali na kusema Serikali haiwezi kukubali uzembe huo kwani imesababishwa na mkandarasi kutokuweka alama za kutosha barabarani wakati akifanya matengenezo.

"Kwa hili kamwe siwezi kukubali watu wafe, tena kwa uzembe, hivyo nakuagiza RTO (Mkuu wa Tradiki Mkoa) mkamate yeye pamoja na vibarua waliokuwa wamechimba shimo hili lililosababisha ajali mara moja. Licha ya kwamba ni rafiki yangu, ila mweke ndani, hatuwezi kuwa tunaangalia tu huu uzembe, nasema kamata weka ndani wote," alisema Simbachawene.

Baada ya kutoa maelekezo hayo, RTO Mkoa wa Dodoma, Nuru Selemani, alimkamata mkandarasi huyo na kumpeleka katika gari la Polisi lililokuwapo eneo hilo. Simbachawene alisema Jeshi la Polisi na Wakala wa Barabara (Tanrods) wanatakiwa kutafakari utendaji kazi wao kutokana na uzembe huo.

"Nuru (RTO), hii ni aibu huu ni zaidi ya uzembe, mashimo yanachimbwa bila kuwekwa alama yoyote,Tanroads mpo tu mnawaangalia... hapa zimetokea zaidi ya ajali nne mnaangalia tu hapana, nasema hapana lazima watu wawajibishwe, nimekasirika mno ," alisema.

Wakati Simbachawene akiendelea kuzungumza, alifika Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Seleman Jafo, na kuonyesha kusikitishwa kutokana na kutokuwekwa alama katika eneo hilo. Mkandarasi aliyekuwa akikarabati eneo hilo, Mohammed Nangonga, akizungumza mbele ya Sombachawene, alisema wamekuwa wakiweka alama, lakini wezi wamekuwa wakiziiba, hivyo kuwapa wakati mgumu.


bgtl BEST GROUP (T) LIMITED
Debts collectors, Auctioneer, Commission Agent, Court Broker & Legal Consultant

**NOTISI NA TANGAZO LA MDANA**

Kwa Idhini tuliyopewa na **BANK OF AFRICA** Tunatoa notisi ya siku kumi na nne (14) kuanzia Tarehe ya Tangazo hili kwa mdaiwa anaetajwa hapo chini, alipe deni analodaiwa na benki hiyo. Kushindwa kulipa kwa muda huo tutalazimika kuuza dhamana (mali) iliyodhamini mkopo huo kwa **MNADA WA HADHARA.** Mnada utafanyika kuanzia saa 4:00 Asubuhi na kuendelea mahali dhamana ilipo kama inavyoonesha hapo chini.

| Na. | JINA LA MDAIWA | MAELEZO YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO |
|---|---|---|
| 1. | JANUARIUS OTTO MKINGA | Nyumba ya makazi yenye kiwanja na.188, Kitalu "**C**" Iliyopo Mbezi beach Dar es salaam kwa jina la **JANUARIUS OTTO MKINGA** |
| 2. | HAMRABI KISEHNA HANGAYA | Nyumba ya makazi yenye hati na.25871, ardhi na.404532, Kiwanja na.477, Kitalu'A", Maeneo ya nyasaka Mwanza iliyopo kwa jina la **HAMRABI KISEHNA HANGAYA** wa sanduku la posta 381,Mwanza |
| 3. | NYANDA & COMPANY LTD | Nyumba ya makazi yenye hati na.18447, Ardhi na.243179 Kiwanja na.430, kitalu 'A" iliyopo eneo la Buswelu Mwanza iliyopo kwa jina la **JOSEPH EDWARD KAHEZELAH NSUMBA** wa sanduku la posta 506,Mwanza |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Dhamana itauzwa kama ilivyo.
2. Mnunuzi atatakiwa kulipa siku ya mnada asilimia 25% ya bei iliyofikiwa.
3. Malipo ya asilimia 75% yalipwe ndani ya siku kumi na nne (14). Kukamilisha malipo yote. Kushindwa kufanya hivyo mnunuzi atakuwa amepoteza malipo yote ya awali ya asilimia 25%, na mnada kurudiwa.
4. Gharama za kuona, kukagua, kuhamisha umiliki, kumtoa mdaiwa/mpangaji na zingine zinazoambatana na hilo ni jukumu la mnunuzi.

Kwa Taarifa zaidi wasiliana na:
Mkurugezi Mtendaji
Best Group (T) LTD
Alli Hassan Mwinyi Road.
Green Acres Buliding, 2nd Floor.
P.O. BOX 1088
DAR ES SALAAM
MOBILE + 255 715-363537/ +255 765-363537

AU

Mkurugezi Mtendaji
Bank of Africa
Head Office,
NDC Development House, ohio street-kivukoni
P.O. BOX 3054,
DAR ES SALAAM
Tel: +255-22-2110104/2111290
Fax: +255-22-2113740

157037


# Wapya 29 wabainika kuwa na corona

**Na Mwandishi Wetu**

IDADI ya watu walioambukizwa ugonjwa wa virusi va corona nchini imezidi kuongezeka kutoka 53 hadi 88 kufikia jana jioni.

Taarifa iliyotolewa na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, ilieleza kuwa idadi hiyo ni kutokana na ongezeko la wagonjwa wapya 29 waliothibitika kuwa na ugonjwa huo.

Taarifa hiyo ilieleza kuwa kati ya wagonjwa hao wapya, 26 wapo jijini Dar es Salaam, wawili wapo Mwanza, na mmoja yupo mkoani Kilimanjaro, wote wanaendelea na matibabu chini ya watalaamu wa afya.

Ilieleza kuwa ufuatiliaji wa watu waliokuwa karibu na wagonjwa hao unaendelea.

"Hivyo, hadi kufikia leo, jumla ya watu 88 wamepata maambukizi ya ugonjwa wa corona nchini kutoka 53 tuliowatolea taarida awali. Ongezeko hili linajumuisha wagonjwa wapya sita waliotolewa taarifa na Waziri wa Afya Zanzibar leo," ilieleza taarifa hiyo.

Ilieleza kuwa wagonjwa walliopona ugonjwa huo ni 11, vifo vikiwa ni vinne.

"Katika kipindi hiki ni muhimu wananchi kuepuka misongamano na mikusanyiko isiyokuwa ya lazima," ilieleza taarifa hiyo.

Aidha, kupitia taarifa hiyo, serikali iliwataka wananchi kuchukua tahadhari ya kujikinga na ugonjwa huo kama taarifa na elimu inavyotolewa mara kwa mara kupitia njia mbalimbali.

# Ajira 45,000 zaja serikalini

**Na Sanula Athanas,** DODOMA

SERIKALI imesema inatarajia kuajiri watumishi wapya 44,811 katika mwaka ujao wa fedha.

Mpango huo ulibainishwa jana bungeni jijini hapa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais - Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Kapteni mstaafu George Mkuchika, alipowasilisha hotuba kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya wizara yake kwa mwaka ujao wa fedha.

Waziri huyo alisema ajira hizo zitagusa kada ya elimu itakayopata waajiriwa wapya 13,529, afya 10,467, kilimo, mifugo na uvuvi 2,145, Jeshi la Polisi 2,725, Magereza 685, Jeshi la Zimamoto 501, Uhamiaji 495 na hospitali za mashirika ya kidini na hiari 1,262.

Vilevile, Mkuchika alisema serikali inatarajia kuajiri watumishi 13,002 wa kada nyinginezo wakiwamo wahadhiri wa vyuo vikuu vya umma nchini na kupandisha vyeo watumishi 222,290 wa kada mbalimbali kulingana na maelekezo yatakayotolewa.

Alisema wizara yake pia itachambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma 20,027 yenye thamani ya Sh. 45,743,803,190.79 (bilioni 45.744) na kuchukua hatua ipasavyo.

Mkuchika pia alilieleza Bunge mafanikio ya wizara yake kwa mwaka huu wa fedha, akibainisha kuwa kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru), wameokoa Sh. bilioni 50.8 kutokana na operesheni mbalimbali za uchunguzi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo unaofanyika kote nchini.

Alifafanua kuwa kati yake, Sh. bilioni 6.7 ni fedha taslimu zilizorejeshwa serikalini, Sh. bilioni 11.2 ni thamani ya mali zilizotaifishwa ambazo ni nyumba tatu na viwanja vinne na Sh. bilioni 30 zilizokolewa baada ya uchunguzi kufanyika na kubaini mzabuni aliongeza bei kwenye huduma aliyotoa serikalini na Sh. bilioni 2.9 zilidhibitiwa au kurejeshwa kwa wananchi.

"Aidha, kiasi cha fedha na mali zilizowekewa zuio kusubiria kukamilika kwa taratibu za kisheria za utaifishaji, ni Sh. bilioni saba, Dola za Marekani milioni 5.26; magari 14 yenye thamani ya Sh. milioni 635, nyumba 14 zenye thamani ya Sh. bilioni 13 na nyumba moja yenye thamani ya Dola za Marekani 410,000," alibainisha.

# Kibaha walia bei ya sukari

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

BAADHI ya wafanyabiashara mjini Mailimoja, Kibaha mkoani Pwani, wamelalamikia kuadimika kwa sukari sokoni.

Aidha, wamelalamika kuwa hata walio nayo wameipandisha bei hadi Sh. 3,000 kwa kilo kutoka Sh. 2,500.

Nipashe ilitembelea baadhi ya maduka katika eneo la Maili Moja na kubaini kuadimika kwa sukari, huku wafanyabiashara wakiwa hawajui wapi wataipata.

Issa Omari na Adinani Mmari, walisema, kwa mara ya mwisho walinunua sukari kwa Sh. 130,000 kwa mfuko wa kilogram 50 kabla ya kuadimika kabisa.

"Hapa kwangu sina sukari, niliyonunua mara ya mwisho kwa Sh. 130,000 imeisha, na sijajua nitaipata wapi, nimejaribu kupiga simu ninakochukulia mara zote, lakini wamesema hakuna, sijajua hatima ya hili ni lini" alisema Mmari

Mwenyekiti wa wafanyabiashara Mkoa wa Pwani, Abdallah Ndauka, alithibitisha kupokea taarifa za ukosefu wa sukari dukani na kuiomba Serikali kusaidia upatikanaji kwa haraka ili wananchi waondokane na changamoto hiyo.

"Nimepata taarifa ya kukosekana kwa sukari dukani, na hata walionayo wanaiuza kwa Sh. 3,000 ambao ni wachache pia, tunaomba serikali ifanyie kazi suala hili," alisema.

Ndauka alisema: Kama kuna uwezekano wafanyabiashara wakubwa waruhusiwe kuingiza sukari kutoka nje kwa kiwango chao ili kuepusha adha ambayo ipo kwa sasa.

Mwanahawa Hamis, mmoja wa wakazi wa Maili Moja, alikiri kununua sukari kwa Sh. 3,000, na kuwa alizunguka kwa muda mrefu kuisaka bidhaa hiyo.



Askari wa Kikosi cha Usalama barabarani, Koplo Mrisho, akiwa chini ya basi la abiria lenye namba za usajili T 488 DGP, wakati akifanya ukaguzi wa magari katika kituo kidogo cha mabasi, mjini Shinyanga jana. Kushoto ni Mkuu wa kikosi hicho, mkoa wa Shinyanga, Africanus Sulle. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Chadema yawapa neno viongozi wa dini corona

**Na Elizabeth Zaya**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) Kanda ya Pwani, kimetoa wito kwa taasisi za dini nchini kuchukua hatua zaidi katika vita dhidi ya ugonjwa wa corona.

Taarifa yake yake kwa vyombo vya habari iliyotolewa na Ofisa Habari wa Kanda hiyo, Lyenda Bernard, alisema chama hicho kinathamini mchango mkubwa unaofanywa na taasisi za dini katika kuhubiri amani na utulivu katika jamii, lakini katika kipindi hiki cha mapambano dhidi ya ugonjwa huo, kuna haja ya kuchukua tahadhari. "Chadema Pwani tunathamini kwa kiwango kikubwa kazi kubwa iliyotukuka inayofanywa na taasisi za dini kuhubiri amani, utulivu na kufariji wananchi katika nyakati tofauti za maisha yao ili kujenga taifa la watu wenye hofu ya Mungu, wenye kutii na demokrasia na kuthamini haki za kila raia," alisema Bernard na kuongeza: "Tunapenda kuchukua fursa hii kwa moyo wa unyenyekevu kuwaomba viongozi wetu wa dini waone kuna haja ya kupunguza mikusanyiko kwenye nyumba za ibada ili kuepuka maambukizi ya virusi vya corona." Taarifa hiyo ilisema kwamba wameamua kutoa wito huo kwa taasisi za dini, baada ya kushuhudia msongamano mkubwa wa watu katika ibada ya Jumapili ya Pasaka. "Wakati Watanzania wakijazana kanisani, makao makuu ya Kanisa Katoliki Vatican kwenye makao makuu ya Kanisa Kuu la Mtakatifu Petro, waumini walizuiwa kuhudhuria misa na kushauriwa wafuatilie kwenye mitandao na runinga."

"Lakini pia mahali patakatifu pa Waislamu kwenda kufanya hija Mecca nchini Saudi Arabia, pamesitishwa huduma ili kupusha msongamano unaohatarisha kusababisha maambukizi ya ugonjwa huo." Aliwaomba Watanzania,kujifunza namna nchi nyingine zinavyochukua tahadhari kupambana na ugonjwa huo.

"Kama Vatican na Mecca wameguswa kwa kiwango hicho, sisi Watanzania tunapaswa pia kuchukua hatua na kuepusha mikusanyiko," ilisema taarifa hiyo ya Chadema

# Jenereta, televisheni vyaibwa hospitalini

**Na Mwandishi Wetu,** PEMBA

MAMLAKA ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) Kisiwani Pemba, inaendelea kuwahoji mfanyakazi mmoja baada ya mwingine wa Hospitali ya Chake Chake, kufuatia tuhuma za wizi wa genereta na televisheni nne.

Imeelezwa kuwa vifaa hivyo viliyoibwa vilikuwamo kwenye wodi ya wagonjwa.

ZAECA, imesema baada kupokea taarifa ya tukio hilo la wizi, iliamua kufuatilia kwa kina kuhusu wizi wa jenereta hilo, baada ya sehemu yake lilipowekwa kukutwa patupu sambamba na televisheni nne nazo kutoonekana.

Mdhamini wa ZAECA kisiwani humo, Suleiman Ame Juma, alisema, baada ya kujiridhisha juu ya wizi huo, wameshaanza uchunguzi unaoambatana na upigaji wa picha wa maeneo vilipokuwapo vitu hivyo.

Alisema jingine ambalo kwa sasa wanaendelea nalo ni kuwahoji baadhi ya wafanyakazi wa hospitali hiyo, ili kupata taarifa na kumtafuta aliyehusika na wizi huo wa mali za serikali kisha sheria kuchukua mkondo wake.

Mdhamini huyo alifafanua kuwa, ZAECA haina nia ya kumuonea mtu yeyote asiyehusika na tukio hilo, ingawa pia hatovumiliwa yeyote aliyehusika na wizi huo bila ya kujali cheo au umaarufu wake.

Katika hatua nyingine Mdhamini huyo ZAECA kisiwani Pemba, alisema inaonesha wizi huo ulifanyika kwa muda mrefu katika hospitali hiyo.

Daktari dhamana wa hospitali hiyo, Ali Omar Khalifa, alithibitisha kutokea kwa wizi huo, ingawa alisema hawajamfahamu aliefanya tukio hilo, ingawa taarifa wameshazifikisha Polisi.

Alisema, jenerata hilo ambalo hawalioni kwa takribani miezi sita sasa, halikuibwa sambamba na televisheni nne, na kuwa moja ilikuwa getini, wodi ya watoto wanawake na wodi ya wanaume.

Alieleza kuwa, wizi wa jenereta hilo lililokuwa kwa ajili ya kusimbazia umeme wa dharura eneo la Thieta, umeathiri utendaji wa kazi kwenye maeneo hayo, hasa umeme wa ZECO unapozimwa wakati upasuaji unaendelea.

# Ujenzi mahakama 33 wilaya wanukia

WIZARA ya Katiba na Sheria, imesema Mshauri Elekezi, ameshafanya mapitio ya michoro ya ujenzi wa mahakama za wilaya 33 zinazotarajiwa kukamilika Desemba mwaka huu.

Hayo yalibainishwa jana na Wizara hiyo ilipokuwa ikijibu swali la Mbunge wa Iramba Mashariki (CCM), Allan Kiula.

Katika swali lake, Mbunge huyo alisema wananchi wa Jimbo la Iramba Mashariki wanasafiri umbali mrefu na pia kutumia gharama kubwa kufuata huduma ya Mahakama ya Wilaya iliyopo Kiomboi na baadhi yao hukata tamaa na hivyo hupoteza haki zao.

"Je, ni lini mahakama ya wilaya itajengwa Mkalama kama ilivyoahidiwa bungeni mwaka 2019?" alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilisema uhaba wa majengo ni moja ya kero inayoikabili Mahakama ya Tanzania.

"Mahitaji ya majengo ya kuendeshea shughuli za Mahakama hapa nchini ni makubwa, kwa msingi huu, Mahakama imejiwekea utaratibu wa kujenga majengo haya kwa awamu kulingana na mpango wa ujenzi na upatikanaji wa Fedha," ilisema.

Ilibainisha kuwa ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya ya Mkalama ni miongoni mwa majengo ya mahakama za wilaya 33 ambayo yatajumuisha Mahakama za Mwanzo katika jengo moja.

"Ujenzi wa majengo haya umepangwa kuanza mwezi Juni na kukamilika mwezi Disemba, 2020 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia," ilisema.

Hata hivyo, ilisema kwa sasa Mahakama ipo katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za awali ili ujenzi wa majengo hayo uanze kwa muda kama ilivyo katika mpango wa Mahakama.

"Tayari Mshauri Elekezi amefanya mapitio ya michoro na ujenzi unatarajiwa kuanza kama ilivyopangwa. Hivyo, ninaendelea kumuomba Mheshimiwa Mbunge kuwa na subira ili jengo hili likamilike ambalo litatatua changamoto alizozitaja," ilisema.

# Dar, Arusha vinara wagonjwa wa figo

MIKOA ya Arusha na Dar es Salaam, imetajwa kuongoza kuwa na wagonjwa wengi wa figo nchini.

Hayo yalibainishwa jana bungeni, na majibu yaliyotolewa na Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto katika swali la Mbunge wa Viti Maalum (CUF), Mgeni Jadi Kadika.

Katika swali lake, alisema ugonjwa wa figo unakua kwa kasi kubwa sana nchini.

"Je, ni mkoa gani katika mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani unaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi wa figo?" alihoji.

Katika majibu ya Wizara hiyo, ilielezwa kuwa tatizo hilo ni kubwa kwa Mkoa wa Dar es salaam ambako takwimu za kitabibu zinaonyesha kuwa na wagonjwa 1,234.

Pia, ilisema mkoa wa pili kuwa na tatizo la wagonjwa wengi wa figo ni Mkoa wa Arusha wenye idadi ya wagonjwa 563 na mkoa ambao una takwimu chache za wagonjwa wa figo ni Simiyu wagonjwa 113.

Awali, Wizara hiyo ilifafanua ugonjwa wa figo husababishwa kwa kiasi kikubwa na magonjwa yasiyoambukiza.

Ilisema utafiti ulioitwa "Community Base Survey to assess prevalence of kidney diseases mwaka 2013" uliofanyika katika maeneo ya Kaskazini Mashariki uliohusisha mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Morogoro pamoja na utafiti uliofanyika mwaka 2015 uliohusisha mikoa ya Pwani na Dar es Salaam, ulionyesha asilimia 44 inasababishwa na ugonjwa wa kisukari.

Pia, ilisema shinikizo la damu linachangia asilimia 34.

"Utafiti huo uliofanyika katika mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Morogoro mwaka 2013 ulionyesha tatizo kuwa kubwa asilimia 7 na takwimu za utafiti kwenye jamii uliofanyika Kisarawe na Dar es Salaam mwaka 2015, ulionyesha tatizo kuwa kwa asilimia 12.4," ilielezwa katika majibu ya wizara.

Wizara hiyo ilibainisha kuwa, magonjwa yasioambukiza husababishwa na mtindo usio bora wa maisha ikiwa ni pamoja na matumizi ya pombe kupita kiasi, matumizi ya tumbaku na bidhaa zake, matumizi ya chumvi ya mezani, kutokufanya mazoezi na kwa ujumla na lishe mbaya, mfano matumizi ya mafuta kupita kiasi.

"Viashiria vyote hivi huchangia kupata magonjwa ya shinikizo la damu na kisukari ambayo ndio husababisha zaidi ugonjwa wa figo. Pia mtindo usiofaa wa maisha upo mjini na vijijini pamoja na mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani," ilisema.

Ilitoa wito kwa wananchi kuendelea kufanya mazoezi kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Selemani Jaffo, akizungumza bungeni jijini Dodoma, juzi. **PICHA: OWM**

# Serikali yaidhinisha aina mpya tisa mbegu za alizeti

BUNGE limeelezwa kuwa, katika kuongeza uzalishaji wa mbegu za alizeti mwezi Desemba 2019, Serikali imeidhinisha aina mpya tisa za mbegu ya zao hilo zenye sifa ya kutoa mafuta mengi kati ya asilimia 32 hadi 42.

Pia, mbegu hizo zinatoa kiwango hicho kwenye mavuno kati ya tani 2 hadi 5 kwa hekta na kuhimili magonjwa na ukame.

Wizara ya Kilimo ilitoa majibu hayo jana bungeni katika swali la Mbunge wa Serengeti (CCM), Marwa Ryoba, ambaye alisema baada ya zao la tumbaku kukosa soko na mwelekeo, wananchi wa Wilaya ya Serengeti wameamua kuanzisha kilimo cha alizeti.

"Je, Serikali iko tayari kuwapa mbegu bora za kisasa zinazotoa mafuta mengi?" alihoji.

Kwa mujibu wa majibu ya Wizara hiyo, serikali imeidhinisha mbegu hizo tisa mpya zinazotoa mafuta mengi.

Aidha, ilisema kupitia Wakala wa Usambazaji Mbegu Tanzania (ASA) na kampuni binafsi itaendelea kuzalisha mbegu hizo pamoja na mbegu aina ya RECORD kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa mbegu za alizeti nchini.

Ilikiri kuwa wakulima wa tumbaku katika Wilaya ya Serengeti pamoja na uzalishaji wa zao hilo wamejikita pia katika uzalishaji wa zao la alizeti ili kuongeza kipato na kuwa na zao la biashara zaidi ya tumbaku.

"Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti imenunua mbegu za alizeti kilo 400 aina ya Hysun 33 zenye thamani ya Sh. milioni 12 na kuwanufaisha wakulima 400 katika kata 10," ilisema.

Aidha, ilisema mbegu hizo zina uwezo wa kuzalisha kilo 800 hadi 1,000 kwa ekari.

"Katika mwaka 2019/20 Halmashauri hiyo pia imetenga jumla ya Sh. milioni 10 kwa ajili ya kununua kilo 300 za mbegu bora za alizeti ambapo taratibu za ununuzi zimekamilika na mbegu hiyo itasambazwa kwa wakulima," ilisema.

Vile vile, ilisema msimu wa 2020/21 Halmashauri ya Serengeti imetenga jumla ya Sh. milioni 25.15 kwa ajili ya ununuzi wa mbegu za alizeti kilo 838.

Kadhalika, ilisema uhamasishaji wa sekta binafsi kushiriki katika kununua na kusambaza mbegu bora za alizeti kwa bei nafuu unaendelea sambamba na uwekezaji katika viwanda vya kusindika alizeti ambapo hadi Machi 2020, kuna jumla ya viwanda sita vya kusindika alizeti vinavyofanya kazi.




**Habari zote na Augusta Njoji,** DODOMA

# ama




Ukurasa 12

**Ijue corona ilivyo ugonjwa wa kinababa**


Ukurasa 13

Changamoto corona ya Afrika na taarifa zake


Ukurasa 14

**Atoka wodini fikra'mpya'dhidi ya aliyokataa hospitali za serikali**

AFYA

# RC Singida: Tumeshaweka 'silaha kifuani' vita ya corona

**Na John Mapepele,** Singida

CORONA inatisha duniani. Hadi jana asubuhi nchini Tanzania kulikuwa na jumla ya wagonjwa 53.

Inaelezwa kiwango si kikubwa sana ikilinganishwa na kwingineko duniani, huku Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) hapa nchini, Dk. Tigest Katsela Mengestu, ameipongeza serikali kwa hatua inazozichukua kukabiliana nayo.

Singida, mkoa ulio kitovu cha nchi, wenye barabara zote kuu zinazounganisha nchi, Mkuu wa Mkoa, Dk. Rehema Nchimbi, anasema wameshawakutanisha wadau wa afya; viongozi wa dini, wataalamu afya, wafanyabiashara na vyombo vya habari, ili kuweka mkakati wa kuukabili na kuzingatia masharti yaliyotolewa na serikali.

"Jambo la msingi kwa sasa katika mkoa wetu wa Singida ni kuwawezesha wananchi wetu kuwa na uelewa wa kutosha wa ugonjwa huu, ili wajikinge kirahisi kabisa na hiyo ndiyo silaha yetu kubwa ya kwanza," anafafanua Mkuu wa Mkoa, anayewaomba wananchi, pia kumkumbuka Mungu.

Kingine kinachotekelezwa, ni kutolewa elimu kwa njia tofauti, vikiwamo vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.

Mganga Mkuu wa Mkoa, Dk. Victorina Ludovic, anasema kila halmashauri imetenga chumba maalum cha kuhudumia watakaohisiwa na corona, wakati wakisubiri taratibu kitaifa za uchukuaji sampuli za uchunguzi. Kituo cha Afya Sepuka, mjini Singida kimetengwa kuhudumia wagonjwa wa mkoa.



Mkuu wa Mkoa Singida, Dk. Rehema Nchimbi (kulia). **PICHA: JOHN MAPEPELE.**

> **Niwaombe ndugu Watanzania kwa ujumla wa madhehebu yote, huu ndio wakati mzuri sana wa kumtegemea Mungu kuliko wakati wote.**

Dk. Rehema anafafanua kwamba, kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, wameshatoa mafunzo maalum kwa wataalamu ambao nao wameshaenda kuwafundisha wa ngazi za chini, namna ya kukabiliana na ugonjwa huo.

Mkuu wa Mkoa anawataka wazazi wote kuhakikisha watoto na wanafunzi wote mkoani wasizurure ovyo, katika kipindi shule zimefungwa, badala yake wajisiomee majumbani.

Pia, anasisitiza ameshaelekeza kila kaya, taasisi, sehemu za biashara na vituo vya mabasi, kuwa na miundombinu ya kunawa mikono na vitakasa mikono (sanitizers) na anatawaka watengenezaji vitakasa mikono mkoani, waandae vingi pasipo kupandisha bei, kwani atakayekiuka atachukuliwa hatua za kisheria.

Dk. Nchimbi anashauri wanakaya, mwenzao anaopotokea kuhisiwa mgonjwa, wamchague wa kumhudumia, ili kupunguza msongamano hospitalini atakapohudumiwa.

Anayooshea kidole mila na tabia za kuendekeza unywaji pombe za kienyeji kwa makundi katika chombo kimoja, akiagiza hilo likome mara moja

Dk. Nchimbi, pia anawaelekeza wamiliki wa nyumba za kulala wageni, kuchukua taarifa sahihi za wageni wanaoingia na kutoka, ili wajue hali zao zilivyo na wanapobaini mgeni ana dalili za corona, taarifa itolewe mara moja.

Huku akisisitiza ni msimu wa uuzaji vitunguu kimkoa, unaoendana na wageni wengi wafanyabiashara kutoka ndani na nje ya nchi, anafafanua agizo lake kwamba:

"Kila mkazi wa mkoa wangu awe mlinzi wa mwenzake ili tuudhibiti kabisa uingiaji na usambaaji wa ugonjwa huu."

Rais Dk. Dk.John Magufuli, ameendelea kutoa elimu ya ugonjwa huo kupitia njia mbalimbali na kuwaondoa hofu wananchi na alipotoa salamu kwenye Ibada kanisani jijini Dodoma, wiki tatu na nusu zilizopita akisema.

"Watu tusitishane, kwa maana, tunatishana mno, anatamka Rais na kuongeza: "Niwaombe ndugu Wakristo na Watanzania kwa ujumla wa madhehebu yote, huu ndio wakati mzuri sana wa kumtegemea Mungu kuliko wakati wote, tuendelee kuchapa kazi, tuendelee kuujenga uchumi wetu"

Hivi karibuni, mtaalamu wa uchumi, Profesa Honest Ngowi, kutoka Chuo Kikuu Cha Mzumbe, Kampasi ta Dar es Salaam, anawakumbusha wananchi kuzingatia tahadhari na miongozo inayotolewa na wizara inayohusika na afya, kuhusu corona.

Anatoa mfano, namna inavyojeruhi uchumi wa dunia katika masoko makubwa ya mitaji, kama ya jijini London, Uingereza na New York, Marekani, jambo linalojenga woga kwa wawekezaji kuja hata nchini.

Pia, anafafanua Tanzania, ambayo utalii ni sehemu ya nyenzo ya uchumi wake, inaathirika katika tafsiri inayobeba mnyororo wa utalii.

AFYA

# Ijue corona ilivyo ugonjwa unaomkamata baba zaidi

Na Jackson Paulo

- Unene chanzo, kuendekeza sigara kumo
- Mjamzito, mnyonyeshaji hawajaguswa




Wananchi mitaani katika kampeni ya kupiga vita janga la ugonjwa corona, nchini Marekani. **PICHA ZOTE: MTANDAO**

IMESHAPITA takriban miezi minne tangu kugundulika virusi aina ya corona . Watu ni wengi wanaoambukizwa na wengi wanapoteza maisha.

Wakati huohuo, kuna tafiti zinazoendelea kufanywa kwa lengo la kubaini tabia ya virusi hivyo, pamoja na athari zake kwa watu wa hali tofauti.

Hapo kunatajwa umri, jinsia, afya ya mwili, hali ya ujauzito na unene. Hivi karibuni, uchambuzi wa takwimu za wagonjwa waliothibitika kuwa na virusi na waliokwishafariki dunia, kutokana na covid 19, umeendelea kufanyika na imeonekana kwa kiasi kikubwa, athari za virusi vya corona vinaweza kuwa tofauti, kati ya mtu mmoja na mwingine.

Kitaalamu kumeibuka mjadala 'kwanini huyu anaguswa na yule haguswi?'Hapo kuna majadala unaowahusu wajawazito, watoto wachanga, wanene na tofauti za athari kijinsia.

### WATOTO JE?

Utafiti unaonyesha kwamba, watoto waliowahi kupata maambukizi ya virusi vya corona, wamekuwa wakionyesha dalili za kawaida na wako mbali na kuugua.

"Vichanga hawapo katika hatari kubwa dhidi ya virusi vya corona, kutokana na kile tunaweza kusema hadi sasa," anathibitisha Mwingereza, Dk. Corda.

Anasema, imeonekana watoto wengi wanaambukizwa virusi vya corona, baada ya kuzaliwa au wakati mama yake anajifungua.

"Bado hatuelewi kwanini hili hutokea, lakini ushahidi wa hivi karibuni hadi sasa unaonyesha hivyo na watoto wengi hawatapata dalili zozote au huishia kupata dalili ndogo ndogo tu," anasema.

Tabibu mwingine, anasema mtoto anaweza kupata maambukizi ndani ya tumbo la uzazi, akirejea mfano wa mtoto aliyezaliwa na mwanamke aliyeambukizwa virusi vya corona, alipopimwa, alikutwa na chembe za kinga ya mwili 'antibodies' dhidi ya corona wakati wa kuzaliwa.

Kwa kawaida chembe za kinga ya mwili au 'antibodies' haziwezi kusafiri kwa njia ya mfuko wa uzazi (placenta) kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto.

Hiyo ina maana kwamba, mtoto alikuwa tayari ameshaanza kupigana na ugonjwa huo tumboni na madaktari wanafafanua, mwanamke aliye na maambukizi ya virusi vya corona, bado anaweza kumnyonyesha mtoto wake kwa sababu hakuna ushahidi kuwa corona inaweza kupitishwa kwa njia hiyo.

### WATU WANENE

Kuna takwimu zinazoeleza kwamba, watu wanene na wenye dhaifu, wako hatarini kupatwa na madhara makubwa zaidi, endapo

> **Daima ni bora kuwa katika hali nzuri kiafya wakati wote.Tunahitaji kupima athari za ugonjwa huu kwanza kutoka kwenye mtazamo wa mtu binafsi.**

wataambukizwa virusi vya corona.

Katika hilo, wanaaswa kuwa makini kujenga mwili wao, ikiwamo kufanya mazoezi na kuuweka mwili katika hali njema kiafya, kama alivyotamka daktari mmoja bingwa.

"Daima ni bora kuwa katika hali nzuri kiafya wakati wote.Tunahitaji kupima athari za ugonjwa huu kwanza kutoka kwenye mtazamo wa mtu binafsi. Hili ni pamoja na kuuweka mwili sawa na kupunguza uzito," anasema.

Takwimu kutoka Shirika la Huduma ya Afya nchini Uingereza (NHS), zinaonyesha asilimia 38 ya waliolazwa katika chumba cha uangalizi maalumu (ICU) kutokana na virusi vya corona ni watu wanene.

Pia, katika wagonjwa waliolazwa ICU, wastani wa nusu yao (55%) walifariki. Kwa wenye unene uliopitiliza na umri wao unazidi miaka 60, kiwango cha vifo vyao ni kikubwa zaidi.

Profesa Fredrik Karpe, wa Chuo Kikuu cha Oxford, Uingereza, anataja mkasa wa wanene kuugua akifafanua: "Ikiwa una tumbo kubwa, basi wakati unalala uzito wa tumbo husukuma 'diaphragm'(kifua na ubavu)kuelekea juu, hivyo kupunguza ukubwa wa eneo la mapafu kutanuka ili kuweza kuingiza hewa ya kutosha.

Inalaezwa, virusi vya corona vinapambana na ufanyaji kazi wa mapafu pekee, hivyo chochote kinachoathiri mfumo huo, kinachangia tatizo kubwa la kiafya.

Profesa Karpe anatahadharisha kuwa, kila mtu anaweza kuambukizwa virusi vya corona na njia bora ya kujihami ni kuandaa mwili katika hali nzuri na imara.

Anawashauri watu wanene kuanza na mazoezi ya kutembea, kuwa na mpangilio mzuri wa chakula, hali inayoipa uwezo mapafu ndani ya wiki mbili, yajijenge zaidi.

### WANAUME HATARINI

Takwimu za kimataifa zinaonyesha, wanaume huugua zaidi kuliko wanawake. Taarifa kutoka Kituo cha Ukaguzi na Utafiti (ICNARC), Uingereza zinaonyesha kibababa wanachukua asilimia 73 kutoka jumla ya wagonjwa zaidi ya 2,000 waliougua corona na kulazwa ICU.

Hadi sasa, taarifa kwingineko duniani katika nchi 18, zinaonyesha idadi ya waliopimwa na kukutwa na maambukizi ya corona ipo juu, ni takriban sawa kati ya wanaume na wanawake, ingawa wanaume wengi zaidi ndio wanafariki.

Nchini Ugiriki na Peru, asilimia 72 ya waliokufa kutokana na corona ni wanaume, wakati Italia, asilimia 68 ya vifo ni kwa wanaume.

Katika nchi za China, Denmark



Ndivyo ilivyo miili ya wanaume, inayotajwa hatari kwa kuugua corona.

na Ujerumani, asilimia 64 ya vifo vinahusu wanaume, huku Uingereza takwimu mpya bado hazijatolewa kuhusu athari za corona, tangu mwishoni mwa mwezi Machi.

Pia, asilimia 61 ya vifo 6,000 vyawali ni vya wanaume. Hapo ndipo inazua swali kuu, kwanini wanaume?

Iligunduliwa kwa mara ya kwanza nchini China, janga lilikoanzia, katika mikasa 44,672 ilivyothibitishwa hadi Februari 11 mwaka huu, wastani wa vifo vilivyowaangukia wa kwa wanaume wote ilikuwa asilimia 2.8 na asilimia 1.7 wanawake.

Wataalamu wakati huo walijiuliza sababu kama mtindo wa maisha kati ya wanaume na wanawake, inaweza kuchangia hilo?

Nchini China, kuna wastani wa nusu ya wanaume ni wavuta sigara na wanawake ni chini ya asilimia nne.

Hivyo, katika mantiki wanaume wako hatarini kuugua magonjwa ya mapafu, moyo, shinikizo la damu na saratani, ambapo zote zinachangia mateso zaidi kwa mgonjwa.

Hata hivyo, maelezo hayo hayakuendelea kuaminika zaidi, pale corona ilipoanza kuingia katika mataifa ya Ulaya, ambako kiwango cha uvutaji sigara ni chini kulinganisha na China, kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani.

Pia, katika uhalisia wanaume wanajulijkana kuwa jinsia dhaifu zaidi linapokuja suala la kupambana na virusi, ikithibitishwa na mkasa wa kuenea virusi vya Sars mwaka 2003, iliyoua watu 780 duniani.

Hadi jana, mtandao wa Worldometre, unaonyesha ugonjwa ulishaua wastani wa watu 126,848 kutoka jumla ya watu 2,005,848 walioambukizwa. Waliopona ni 486,874.

Sars, nayo inaonyesha ilikuwa mbaya zaidi kwa wanaume, kwani asilimia 21 ya waoambukizwa walifariki, ikilinganishwa na wanawake asilimia 13.

Katika taarifa hiyo, kurejea mtandao wa Johns Hopkins, ambayo inataja vyanzo vya Shirika la Afya Duniani (WHO) hadi kufikia Jumanne iliyopita, jumla ya watu 15, 471 walishaambukizwa, kati yao 2,953 walishapona na 835 walifariki

Pia, mwaka 2012 kuna asilimia 63 ya kinamama walioambukizwa ugonjwa wa mers walikuwa wanaume.

"Huu ni mwendelezo wa mfanano tuliouona kwa maambukizo mengi ya virusi vya njia ya upumuaji - wanaume wanaweza kupata matokeo mabaya," anasema mtaalamu wa tofauti za jinsia Sabra Klein, mwanasayansi wa Chuo Kikuu cha Johns Hopkins cha Marekani.

"Tumeona hili kwenye aina zingine za virusi, wanawake wanapigania navyo vyema zaidi kuliko wanaume," anafafanua.

Daktari James Gill, anaamini sababu mojawapo ni kwamba wanaume hawatunzi miili yao na walevi kuliko wanawake.

Aidha, utafiti mbalimbali unaonyesha wanaume wana nafasi ndogo kufuata masharti ya lishe bora na sio wepesi kutafuta msaada wa matibabu, hata wanapoihitaji.

Profesa Philip Goulder, mtaalamu wa ya kinga ya mwili, anayetoka Chuo Kikuu cha Oxford, anaeleza, tofauti za kiafya zilizopo ni tabia za athari baina ya jinsia hizo.

Baada ya takwimu kuthibitisha kuwa watu wanene wanaougua, zaidi wanaokufa, mtaluma huyo anafafanua mwanamume ana asili ya umbile la tufaha (apple) katika eneo la katikati ya mwili na tumbo.

Anasema, unene wa tumbo una asili ya kuathiri upumuaji wa mgonjwa na kumuongezea kandamizo kwenye misuli ya upumuaji, hivyo mgonjwa wa corona huwa anashindwa kupumua vizuri.

Wanasayansi wa masula ya vinasaba (DNA) wametoa pia tathimini yao, kueleza kinachosababisha tofauti kati ya wanaume na wanawake.

> **Sars, nayo inaonyesha ilikuwa mbaya zaidi kwa wanaume.**

"Kuna tofauti kubwa kati ya mfumo wa kinga ya mwili kati ya wanaume na wanawake, na kwamba tofauti hizi zina athari kubwa katika kuamua kiwango cha madhara yatokanayo na magonjwa hasa ya kuambukiza,"anasema Profesa Goulder.

Pia, anasema mfumo wa mwitikio wa kinga baada ya chanjo na vita dhidi ya maambukizo ya mwili, mara zote umeonekana mkali na imara zaidi kwa wanawake, ikilinganishwa na wanaume.

***Makala hii imeandaliwa kwa mujibu wa taarifa za kimataifa na mwandishi anapatikana kwa baruapepe:: jacpole@gmail.com***



## Changamoto corona ya Afrika na taarifa zake



Corona jijini Kigali; kampeni ya wasafiri kunawa katika vituo vya basi, wakitumia vyombo vinavyohamishika. **PICHA: MTANDAO**

**Na Michael Eneza**

MTU akiangalia au kutathmini ugonjwa corona au covid 19, kasi inavyoenea barani Afrika na ulivyoanza Marekani na kwingineko, mifumo hiyo inafanana.

Kwa vipi? Yaani mstari wa chati za takwimu zinapanda kwa kasi, mithili ya mchoro wa mgongo na shingo ya twiga anakula majani mtini.

Endapo watu watauliza na watabaki vipi salama, jibu lake ni gumu kutolewa. Maambukizi ya kwanza yalikuwa Machi 17, na wiki tatu baadaye yalifishafika 10,000 duniani.

Swali mojawapo linaloulizwa ni katika mijadala ya kitaaluma ni jinsi mifumo ya sekta ya afya barani Afrika, inaweza kukabiliana na wimbi la homa hiyo, hata kufanana na nchi za Magharibi, ambako hali ni mbaya.

Mitazamo ya wengi inaangukia shaka, kwani chembe ya ndani ya ugonjwa ni kirusi cha mafua halisi, hakiendani na joto la Afrika, kunakoelezwa kuna kasi ndogo ya maambukizi, ingawa bado kunafuka moshi.

Dalili mbaya ya tatizo hilo ni mazingira yanayojitokeza Kusini mwa Afrika, maambukizi yanaanza kuenea katika kipindi cha baridi kikianza, joto likipisha msimu mwezi huu. Ahueni ya joto inatarajiwa kurudi tena mwezi Novemba, ndipo kirusi kianze kukosa nguvu tena.

Hata hivyo, kinachojadiliwa zaidi nje ya nchi, ni uwezo wa Afrika kulibeba janga hilo ama kiafya au kimatibabu.

Kuna msemo wa Waingereza "ignorance is bliss," ikiimaanisha 'kama hujui kuna furaha' kwani kile ambacho kingeweza kukuumiza moyo, huna habari nacho.

Wimbi la corona ni vigumu kulificha. Vifo vinatokea kwa haraka, hasa kwa walio dhaifu kwa njia moja au nyingine. Pia, katika kuhudumia inakuwa ngumu kupata takwimu kila wakati, kukiwepo ugumu wa mapambano yenyewe. Hata mamlaka zenye dhamana hazitakuwa na mbadala. Hapo inajumuisha serikali, zinapoamua kukusanya kwa kipindi fulani, mfano wiki, kisha inaitangaza.

Tayari hiyo imeshatokea kuwa sehemu ya malalamiko nchini Marekani, kwenye mzizi wa tatizo China, kwamba hakuweka kwa usahihi wingi wa maambukizi na mahali penye tatizo lenyewe.

Pia, katika mtazamo wa namna fulani, unadai kwamba Marekani haikujua kama ilikuwa na haja ya kukuchukua hatua za ziada, kwa mtazamo 'ni tatizo la China' kumbe ni ukweli ni kimbunga cha kimataifa kisichojua mipaka au mifumo ya kimataifa.

Hapo ndio panapozaa mtazamo wa mtihani wa serikali za Kiafrika kuhudumia watu wake chakula na mahitaji mengine kwa miezi kadhaa, wakiwa karantini ya lazima.

Nchi za Magharibi zimeshaanza kujadili kwa kina, namna ya kuhakikisha mtu anabaki na akili timamu, endapo atazuiliwa kutoka nje, hasa kama hana shughuli ya maana anayoweza kuifanya kimtandao au kwa simu, nje ya porojo.

Pia, kunatajawa tatizo la magonjwa ya akili. Ubongo wa mtu unahitaji kuangalia kuona njia, mwanga kwa mbali, na siyo hali isiyotabirika kukaa nyumbani bila ya matumaini.

Hadi ilikofikia, corona bado ni kubwa kimataifa na kuna maeneo yanayojongea kiuchumi na kibiashara, kwa uhaba wa walaji (wanunuzi, wateja), pia kupungua shughuli za uchumi, kunakoathiri waliobaki.

Daima, kinachopatikana huwa tatizo zaidi katika mazingira ambako nchi haina mfumo wa vipato vya msingi kwa kila mtu, hasa wasio na ajira. Ni hali inayolazimisha ubangaizaji na kuishia kuzidisha uwezekano wa maambukizi.

Ni dhana inayokumbusha usemi wa Mwalimu Julius Nyerere kwa kauli ya mzaha "It is very expensive to be poor (Ni gharama kubwa kuwa maskini)."

Lingine linalojitokeza kwa kasi katika kuenea homa ya mapafu sasa, ni maskini wanaokaa katika maeneo yaliyobanana, wanakuwa hatarini zaidi kuliko wengine.

Nchini Marekani, wenye asili ya Afrika hawazidi asilimia 13 ya wakazi wote na kuna maeneo, ambako vifo vimetokea wastani unaokaribia unawaangukia weusi.

AFYA

## BORIS JOHNSON;

# Atoka wodini fikra 'mpya' dhidi ya aliyokataa hospitali za serikali

**Na Ani Jozeni**

WACHAMBUZI wa siasa nchini Uingereza, wameanza kuangalia kwa makini mwelekeo wa Waziri Mkuu Boris Johnson kisera, baada ya kuruhusiwa kuondoka Hospitali ya Saint Thomas, mahali alikolazwa hayati Mwalimu Julius Nyerere takriban miaka 21 iliyopita.

Johnson wa kuanzia wiki hii, ni mwingine kabisa dhidi ya msimamo wake wa kisera wa siku nyingi, kuhusu namna ya kuendesha huduma za afya hospitalini.

Boris 'aliyepigiwa chapuo' na Rais Donald Trump wa Marekani kuchukua nafasi ya Theresa May, baada ya hoja ya mkataba wa Brexit kukwama bungeni, alidhihirisha undani wa hisia na uzalendo wake usio wa kawaida.

Hizo ni hisia kuhusu mfumo huduma za afya kitaifa, kwamba ni kielelezo muhimu cha uzalendo nchini Uingereza.

Kihistoria, kutoka mtazamo wa kimataifa katika uongozi wake, Mwalimu Nyerere alikuwa kati ya waliotokea kukubali kimataifa fikra ya kisiasa za kundi la Fabian Society, wenye mwelekeo wa Kijamaa.

Chimbuko la fikra na kundi hilo, ni kupinga yaliyojiri badaa ya mapinduzi ya viwanda nchini Uingereza na kukaibuka kundi la wasio na ajira wakitangatanga na hata waajiriwa, walionyanyasika.

Katika historia hiyo, inayobeba hata chimbuko la vyama vya wafanyakazi duniani na baadhi ya nadharia za taaluma za rasilimali watu, ndio ilibua kundi la kiharakati la Fabian Society, ambalo halikukubaliana na uonevu huo kwa wafanyakazi.

Kimsingi, jadi na fikra zao ndizo kielelezo cha siasa za chama cha Labour nchini Uingereza hadi leo. Viongozi wa chama hicho, akiwamo Waziri Mkuu Harold Wilson, walimuelewa sana Mwalimu, alipotaifisha njia kuu za uchumi mwaka 1967, kupitia Azimio la Arusha.

Boris Johnson, alitoka hospitalini Jumapili na akatoa taarifa aliyoisoma mwenyewe kutoka nyumba ya mapumziko ya Chequers, ambako alisema huduma ya madaktari na manesi, ndizo ziliamua ugonjwa wake unakoelekea.

Kimantiki inaangukia hata tafsiri uwezekano wa kifo ulikuwa mkubwa, kama isingekuwa hatua hizo za kitabibu zilizochukuliwa na madaktari na manesi, alipokuwa katika chumba cha uangalizi maalum (ICU).

Kulikuwapo maelezo yanayolenga kujenga picha kuwa alihudumiwa kama mgonjwa mwingine yeyote na kwa vile alianzia wodini, kisha kuingia ICU na akarudi wodini. Ni jambo linaloingia akili, kwa sababu hapakuwapo chumba maalum alikolazwa wakati wote.




Hii ndiyo hospitali ya St. Thomas, alikolazwa Waziri Mkuu, Boris Johnson, kutokana na maradhi ya corona. **PICHA ZOTE : MTANDAO.**

> **Johnson alikuwa mmoja wa mawaziri (Mambo ya Nje wakati huo) waliojitoa katika serikali ya Waziri Mkuu Theresa May, kupinga makubaliano aliyokuwa anaelekea kufikia na Umoja wa Ulaya (EU).**




Waziri Mkuu, Boris Johnson, akizungumza hospitalini, Jumapili iliyopita, siku ya Pasaka.

Kuingia hospitalini kwa Waziri Mkuu Johnson, kumekuja kabla ya mwaka kukamilika, kuanzia pale utawala wa mtangulizi wake, Waziri Mkuu Theresa May, ulipotangaza Mpango wa Miaka 10 wa Shirika Kuboresha Mfumo wa Afya wa Uingereza (NHS).

Hii ni kabla ya Januari mwaka jana, Rais Trump hajazua upinzani kwamba NHS ibinafsishwe. Alidai ina madeni makubwa na imekwama.

Mwezi Juni, kiongozi huyo wa Ulaya, alifanya ziara fupi nchini Uingereza, akitokea shughuli kikazi katika nchi nyingine za barani Ulaya.

Ni wakati wanachama wa chama cha tawala Uingereza cha Conservative, walikuwa wanaendelea na matayarisho ya kura za maoni kupata kiongozi mpya wa chama hicho bungeni.

Johnson alikuwa mmoja wa mawaziri (Mambo ya Nje wakati huo) waliojitoa katika serikali ya Waziri Mkuu Theresa May, kupinga makubaliano aliyokuwa anaelekea kufikia na Umoja wa Ulaya (EU).

Baadaye, Boris alifikia makubaliano kama hayo, ila EU ilikubali kuendelea na majadiliano, kipengele cha mpaka wa Ireland.

Akiwa ziarani Uingereza, Rais Trump alikuwa anaunga mkono chama cha siasa kali kuikataa kabisa EU, huku washauri wake wa karibu kama John Bolton, akiwaunga mkono wafuasi wa chama cha Kifashisti nchini Italia.

Sera zao ni pamoja na kufuta mifumo ya huduma za tiba kwa hospitali za taifa, kwa hoja kuwa zinapoteza fedha, hoja ambayo zina nguvu kiasi katika siasa za nchini Marekani.

Wanatumia mfumo wa bima,ambao siyo kwa wote wanaozipata, hivyo mtangulizi wake Rais Barack Obama, alipata tabu kutaka kuhakikisha kila mtu anapata bima.

Mpango wa Waziri Mkuu wa awali May, ulikuwa kuingiza kiasi cha Pauni za Uingereza bilioni 20 (wastani Sh. trilioni 50) hadi kufikia mwaka 2023.

Kwa aliyosema Boris, baada ya kutoka hosptalini Saint Thomas, ni wazi mpango huo atautekeleza au kuuboresha endapo ataombwa kufanya hivyo.

Ni hatua inayoweza kubadili mjadala kuhusu Mfumo wa Afya wa Taifa nchini humo na kumaliza ubishi kuhusu athari za kujitoa EU, dhidi ya sekta ya afya Uingereza.

Wengi walitazamia matumizi EU yakipungua, mfumo huo wa afya ungepata fedha zaidi, hadi Rais Trump alipoingia na sera ya kuibinafsisha, ambayo hata hivyo haikuungwa mkono na chama tawala cha Conservative.

Wachambuzi wanakumbusha kuwa, ufashisti Ulaya mara nyingine huendana na Ujamaa kiasi. Kuinua dola na kuvunja nguvu kampuni kubwa zenye kulenga faida na si nchi.

Kuzaliwa upya au "kufufuka"kiitikadi kwa Johnson wakati wa Pasaka baada ya kutoka hospitali, ni habari njema nchini humo, kwamba mivutano ya kiitikadi inawekwa pembeni wakati wa vita ngumu ya Covid-19. Kuugua Johnson kuliishtua nchi, halafu ikawa ahueni kiitikadi.

Kabla hajaingia madarakani, Johnson, alikuwa mmoja wa viongozi wa chama tawala cha Conservative wanaoonekana kuwa na msimamo mkali dhidi ya uendeshaji wa NHS na alivyobadilika sasa, ni kiwango cha neema kwa huduma kwa wagonjwa wa nje (OPDs).

Wakuu wa shirika hilo, wanaisitiza kuwa wakati mpango huo uliojadiliwa bungeni Juni mwaka jana wa kupunguzwa fedha za kuwaangalia wagonjwa wa nje, ili wasihitaji kulazwa zitaumiza ufanisi wa mpango wa miaka 10 wa Theresa May.

Baada ya kutoka hospitalini akiwa na ari mpya kuhusu NHS, huenda Boris Johnson akasikiliza kwa makini zaidi shirika hilo linachotaka kuboresha huduma kwa wananchi wa kawaida, hasa wale ambao hawajalazwa.

Kuzuka kwa kirusi cha Covid-19( corona) kumeleta changamoto isiyopimika sekta ya afya duniani, Uingereza ikijidhirisha kwa sura yake.



## HABARI DODOMA

# Askofu ataka maombi kitaifa kuhusu corona

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

ASKOFU wa Kanisa la Maombezi jijini Dodoma (EHT), Dk. Eliah Mauza, amemwomba Rais John Magufuli, kutangaza maombi maalum ya kufunga na kumuomba Mungu kwa madhehebu yote nchini ili aiepushie Tanzania na janga la ugonjwa wa corona (covid 19).

Askofu Dk. Mauza, aliyasema hayo jana jijini Dodoma wakati akizungumza na waandishi wa habari juu ya janga hilo.

Alisema kuwa upo umuhimu wa wananchi wote bila kujali imani zao, kufunga na kuliombea Taifa na Rais wa nchi pekee ndiye mwenye mamlaka ya kuliambia Taifa kufanya hivyo. "Rais amekuwa mfano kila wakati kuliombea Taifa katika mapambano dhidi ya corona, lakini sasa ni vizuri atamke Taifa lifunge na kuomba ili kumuomba Mungu kwa ajili ya uponyaji dhidi ya corona," alisema Askofu huyo.

Alisema ugonjwa huu ni pigo kwa dunia na ndio maana hata nchi zenye uwezo wa kifedha na vifaa vya kutosha, zimeshindwa kupata tiba, na kuwa muda mfupi umeshaua maelfu ya watu duniani.

Aidha, alitumia fursa hiyo kuwataka viongozi wa Serikali kutopuuza suala la maombi.

"Neno la Mungu linasema 'niangalieni mimi mkaokolewe'...kwa hiyo pamoja na kufuata maelekezo mengine ya kisayansi ya kujikinga na ugonjwa huu, lakini pia maombi ndio dawa ya kuiponya Tanzania," alisema na kuongeza:

"Dunia nzima imetikisika leo hakuna cha daktari bingwa, wote wameshindwa sasa tumtazame Mungu pekee, huku tukitubu kwake."

Alisema Tanzania ni miongoni mwa nchi zinazotenda dhambi, hivyo inapaswa itubu maovu na imgeukie Mungu kwa maombi ili kupata majibu ya ugonjwa huo. Aidha, alisema kuwa majanga kama ya corona siyo mara ya kwanza kuikumba dunia, kwani hata katika vitabu vitakatifu vinaonyesha kuna vizazi vilishakumbwa na ugonjwa wa tauni, lakini kutokana na viongozi wake kufunga na kuomba, maradhi hayo yaliondoka mara moja.



Wananchi wakipita kandokando ya barabara iliyoharibiwa na mvua katika Mtaa wa Chinyoa, Kata ya Kilimani, jijini Dodoma jana, na kusababisha usumbufu kwa watumiaji wa barabara hiyo. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Amfuata Lukuvi bungeni malalamiko kuporwa ardhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKAZI wa kijiji cha Nyahanga, wilayani Kahama mkoani Shinyanga, Magohe Kafumu, amemfuata bungeni jijini Dodoma, Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, William Lukuvi, ili amsaidie kupata haki yake ya ardhi ekari 20 alizonyang'anywa na baraza la ardhi.

Kafumu akizungumza na waandishi wa habari, alisema lengo lake ni kuhakikisha anamfikishia kilio chake waziri huyo kutokana na kukosa msaada katika wilaya yake.

Alisema amekuwa akihangaika kwa muda mrefu kupata msaada katika ngazi tofauti bila mafanikio, na sasa ameamua kufunga safari na kwenda jijini Dodoma ili apate fursa ya kuonana na Waziri Lukuvi.

Alisema eneo analolilalamikia ni la ukubwa wa ekari 20, ambalo alinunua kwa Ilagila Kapagala kwa Sh. milioni 3.5 mwaka 2013.

Alisema kabla ya kulinunua eneo hilo, alikuwa akikodi kwa mwaka kwa gharama ya Sh. 200,000, lakini baadaye mmliki wa eneo hilo akadai kumuuzia.

"Aliposema kuwa anauza nikamuuliza Sh. ngapi, akasema kwa sababu nimekuwa nikikodi basi impatie Sh. 3,500,000, nikaanza kumpatia kwanza milioni moja na baadaye mkewe akaja kufuata nyingine na tulikuwa tukiandikisha kwa mwenyekiti wa kijiji na nakala zote zipo," alisema.

Aidha, baada ya kulinunua na kuanza kulima alipata samansi kutoka Baraza la Ardhi la Wilaya ya Kahama ambapo alikwenda kuitikia wito.

Alisema alipofika aliambiwa hatakiwi kufanya chochote kile katika eneo hilo ambalo alishalima mpunga na kutumia gharama ya Sh. 17,350,000.

Alifafanua kuwa jambo la kushangaza ni namna ambavyo kesi hiyo iliendeshwa kwani katika siku zote za kuhudhuria vikao vya baraza hilo, mlalamikaji hakuwahi kufika hata siku moja wala mashahidi hawakuitwa kutoa ushahidi.

"Hukumu wakatoa wao kuwa natakiwa kuliachia shamba na mpaka Juni mwaka huu natakiwa kutoa vitu vyangu, lakini kinachoonekana ni kuna watu wanalitaka eneo lile, tena kwa bei ya juu na ni viongozi wakubwa wa wilaya yetu,"alisema Kafumu.

Akizungumza kwa njia ya simu aliyekuwa Mwenyekiti wa Kijiji cha Nyahanga, Daudi Samson, alisema katika uongozi wake alishuhudia sehemu ya mauziano ya eneo hilo na kudai kuwa ushahidi wote anao.

"Mimi nikiwa kiongozi sehemu ya mauziano nilishiriki kama mwenyekiti, lakini nashangaa kwa nini sisi kama mashahidi hatujaitwa na mlalamikaji... hakuwahi kwenda katika kesi, lakini uamuzi umetolewa,"alisema Samson.

Mwenyekiti wa Baraza la Ardhi Wilaya ya Kahama, Paulo Lekamoy, alisema kama kuna mtu anaona kuwa haki haikutendeka, akate rufani au aende kokote anakoona kutamsaidia.

"Kama amekuja hapo na anadai anataka kwenda kwa Waziri mwache aende na kama hajaridhika na uamuzi basi akate rufani, sina maneneo mengine ya kusema, nina kazi nyingi za kufanya."

# Wananchi waonywa upotoshaji corona

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WANANCHI wamesisitizwa kuacha kuzusha taarifa kuhusu ugonjwa wa corona, badala yake kufuatilia taarifa sahihi kutoka mamlaka husika.

Angalizo hilo lilitolewa na Dk. Faraja Eliamuya, kwa niaba ya Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma wakati akizungumza na wanahabari.

Alisema kufuatia kuwapo kwa janga la virusi vya corona nchini, wapo watu wachache wasio waaminifu wanaopotosha jamii.

Alisema hadi sasa wataalamu wa afya wanaendelea kufuatilia katika maeneo mbalimbali ya mkoa na pindi itakapobainika kuna mtu mwenye dalili za ugonjwa huo atafikishwa katika vituo vilivyotengwa kupata huduma za kitabibu.

Pia, alisema virusi vya corona hadi sasa vimeenea mataifa mengi duniani na kusababisha vifo, kuyumba kwa shughuli za kiuchumi na baadhi ya mataifa kutoa amri ya raia wake kutotoka nje kuepuka kusambaa kwa virusi, hivyo, kuwataka wananchi kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya.

Mratibu wa shughuli za afya kwa ngazi ya jamii, Marry Kongola, alisema wametoa elimu kwa wananchi namna ya kujikinga na virusi vya corona katika maeneo mengi ikiwamo maeneo ya masoko na nyumba za ibada akieleza kuwa mwitikio umekuwa mkubwa kwa watu kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya jinsi ya kuchukua tahadhari.

"Mwitikio umekuwa mkubwa kila tunapokwenda kutoa elimu jambo ambalo linatia moyo sana," alisema.

Alitoa wito kwa wananchi kutii maelekezo yaliyotolewa na kuwataka viongozi wa Serikali za mitaa katika maeneo yote kusimamia maagizo hayo kwa kuendelea kuhimiza na kufuatilia utekelezaji wake katika maeneo yao.





## Dhamana yakwamisha wajasiriamali mikopo

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

UKOSEFU wa dhamana kwenye mali zisizohamishika ikiwamo nyumba, imetajwa kuwa sababu inayochangia wajasiriamali wadogo katika Halmashauri ya Jiji la Mbeya, kushindwa kunufaika na mikopo inayotolewa na taasisi za kifedha.

Kundi maalumu la watu wenye ulemavu, wanawake na vijana wanakosa fursa ya mikopo kwa sababu baadhi yao hawana biashara za kufanya hivyo kutegemea mikopo kuanzisha biashara.

Hayo yalisemwa jana na mjasiriamali wa mboga na matunda, Yasinta Peter, kutoka soko la Sido. Alisema taasisi za kifedha zimeweka masharti magumu ya utoaji mikopo hasa kwa wanaomiliki nyumba pekee wakidai hawawezi kurudisha mikopo kwa sababu nyumba hazizalishi.

"Tunaomba masharti ya mikopo yalegezwe hata nyumba tunaweza kuziwekea dhamana na tukapata mikopo ya kufanyia biashara, watu wenye ulemavu wanatamani sana kufanya biashara, lakini kwa sababu hawana mitaji wanakosa hiyo mikopo," alisema Peter.

Ashura Mwaipyana, mwenye ulemavu wa miguu, alisema licha ya tatizo alilonalo, lakini anapenda kufanya biashara, kikwazo ni taasisi za kifedha kushindwa kumuamini na kumpatia mkopo ili akuze biashara yake ya karanga aliyoianza hivi karibuni.

Alisema kundi la watu wenye ulemavu haliaminiwi na benki kwa hofu kuwa watashindwa kurudisha fedha suala ambalo alidai ni mtazamo hasi, na kueleza kuwa wao ni waaminifu na wanajituma.

Ofisa biashara wa Jiji la Mbeya, Joseph Seme, alisema wanatoa mikopo yao bila masharti magumu na kipaumbele kwa wajasiriamali walio kwenye kundi maalumu ambao ni watu wenye ulemavu, vijana na wanawake.

Alisema, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Jiji ilitoa mikopo ya Sh. milioni 73 kwa vikundi 21 vilivyosajiliwa kwa mujibu wa sheria.

Aliwaomba wajasiriamali wanaopata mikopo hiyo kuwa waaminifu kurejesha fedha kwa wakati ili zitumike kwa wengine, alisema fedha hizo hazitolewi kama hisani bali zinatakiwa kurejeshwa kwa wakati.

Mkuu wa Wilaya ya Mbeya, William Ntinika, alisema kwa kipindi cha miaka miwili iliyopita, Sh. milioni 218.4 zilikopeshwa kwenye vikundi mbalimbali vya ujasiriamali.

# Polisi yakagua magari yasiyo na vifaa vya kunawa mikono

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

JESHI la Polisi Kitengo cha Usalama barabarani katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, kimeanza ukaguzi wa magari ya abiria yanayofanya safari zake ndani ya wilaya hiyo, kuangalia utekelezaji wa agizo la serikali la kuweka ndoo za maji na sabuni ili kila abiria aweze kunawa mikono zikiwa ni jitihada za kukabiliana na ugonjwa wa Covid-19.

Akizungumza na Nipashe jana wakati wa ukaguzi wa magari pamoja na kutoa elimu kwa abiria na madereva, Mkuu wa Kikosi cha Usalama barabarani wilayani humo, Abel Kidai, alisema suala la kunawa mikono ni lazima kwa kuwa ni agizo la wataalamu katika kukabiliana na ugonjwa huo unaosababishwa na virusi vya corona.

Alisema endapo dereva hataweka ndoo za kunawa mikono pamoja na sabuni au vitakasa mikono kwa ajili ya abiria wanaopanda na kushuka kwenye gari, hatua za kisheria zitachukuliwa ikiwa ni pamoja na kulipa faini au kufikishwa mahakamani.

"Kikosi cha usalama barabarani kimefanya operesheni kwenye vituo mbali mbali vya daladala, lengo ni kuangalia utekelezaji wa agizo la kuhakikisha magari yote yanakuwa na ndoo za maji na sabuni kwa ajili ya watu kunawa mikono, mwitikio bado ni mdogo, lakini naamini utekelezaji bado unaendelea," alisema Kidai.

Alikemea tabia ya baadhi ya abiria kupenda kusimama ndani ya magari na kusababisha mlundiko wa abiria hali inayohatarisha afya za wengine.

Aliwasisitiza madereva kutii agizo la kuhakikisha abiria wote ndani ya daladala wanapata siti.

Mmoja wa madereva, Peter Nestory, alisema ugonjwa wa Covid-19 ni hatari na waliyapokea masharti yote yaliyotolewa na wataalamu wa afya ikiwa ni pamoja na kuhakikisha magari yao yanakuwa na ndoo za maji na sabuni pamoja na kupulizia dawa.

Alisema kikwazo kinachosababisha baadhi yao kushindwa kutimiza masharti hayo ni gharama kubwa za vifaa, kwa madai kuwa hali ya kiuchumi ni ngumu, abiria ni wachache na wamiliki wanahitaji fedha za malengo



Mkuu wa Wilaya ya Mbarali, mkoani Mbeya, Reuben Mfune (katikati), akipata maelezo kutoka kwa Ofisa Afya wa Wilaya hiyo, Said Sadick, kuhusu namna ya kutambua sabuni zinazofaa kutumiwa ili kukabiliana na maambukizi ya virusi corona, alipotembelea eneo la Igawa, hivi karibuni, kuangalia utekelezaji na hamasa ya watu kunawa mikono kwa maji tiririka na sabuni. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Mbegu mpya ya maharagwe yagunduliwa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

KITUO cha Utafiti wa Kilimo Tari, Uyole kilichopo jijini Mbeya, kwa kushirikiana na taasisi nyingine za kimataifa kimegundua mbegu mpya za maharagwe, karanga na soya zenye uwezo wa kukabiliana na tatizo la udumavu kwa watoto pia zikiwa na uwezo mkubwa wa kurutubisha ardhi kwa ajili ya ustawi wa mazao mengine.

Haya yalisemwa juzi na Mkurugenzi wa Kituo cha Utafiti wa Kilimo Uyole, Dk. Tulole Bucheyeki, kuwa utafiti uliofanyika kwa miaka minne ulibaini kuwa Tanzania kuna tatizo la udumavu wa watoto kutokana na kukosa lishe bora, na pia ardhi inayofaa kwa kilimo ikiwa imeishiwa rutuba kiasi cha kushindwa kuzalisha mazao yenye lishe bora.

Dk. Tulole, alisema ugunduzi huo wa mbegu za mazao ya chakula itakuwa msaada mkubwa katika kukabiliana na tatizo la utapiamlo na kituo kitaendelea kuzalisha na kuwauzia wananchi kwa gharama nafuu. "Kwa miaka minne kituo chetu kilijikita kutafuta mbegu mpya za mazao kama maharagwe na karanga ili kusaidia kukabiliana na tatizo la utapiamlo kwa watoto, tumefanikiwa, kazi kubwa iliyopo ni kuongeza uzalishaji na kutoa elimu kwa wananchi namna ya kutumia ili kuwasaidia watoto kuwa na afya njema," alisema Dk. Tulole.

Naye Mwakilishi wa Shirika la kimataifa la Utafiti wa Kilimo, IITA nchini Tanzania, Dk. Fred Kanampiu, alisema tatizo la udumavu kwa watoto linatokana na wazazi kutokuwa na elimu ya lishe bora.

Alisema Shirika hilo kwa kushirikiana na Tari, Kituo cha Uyole, litasaidia upatikanaji wa vyakula tofauti vyenye lishe bora kwa watoto ikiwa ni pamoja na uzalishaji wa mbegu lishe kwa wingi.

Baadhi ya wakulima walisema, ugunduzi wa mbegu hizo ni mkombozi kwao kwa kuwa watalima mazao yatakayokidhi viwango vinavyohitajika kwenye soko la ushindani.





Katibu Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Shaaban Seif Mohamed, akizungumzia na viongozi wa Bandari ya Mkokotoni, manahodha na wakuu wa madiko, wilayani Kaskazini, juzi.

# Vyombo vya usafirishaji bandari bubu kutaifishwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

KATIBU Mkuu Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Shaaban Seif Mohamed, amesema ni jambo la kusikitisha kuona baadhi ya bandari bubu zinaendelea kutumiwa kwa kusafirisha abiria kutoka nje ya Zanzibar, licha ya marufuku ya Serikali.

Alisema marufuku ya Serikali haijatenguliwa na kukumbusha kwamba vyombo vya dola havitasita kuwachukuliwa hatua za kisheria watu watakaokaidi marufuku hiyo na kutaifisha vyombo vitakavyobainika kutumika.

Shaaban alieleza hayo katika kikao kilichowakutanisha viongozi na watendaji wa Bandari ya Mkokotoni, wakuu wa madiko ya uvuvi, manahodha wa vyombo vya baharini, viongozi wa Serikali ya Wilaya ya Kaskazini 'A' kilichofanyika Ofisi ya Halmashauri ya Wilaya hiyo huko Mkokotoni.

Kikao hicho kimekuja kufuatia ongezeko la baadhi ya watu wanaoingia Zanzibar kwa kutumia bandari bubu wakitokea Tanzania Bara, ambao baadhi yao walifanyiwa uchunguzi na wataalamu wa afya na kubainika kuwa na dalili za virusi vya corona.

Alisema kasi ya maambukizi ya virusi vya corona inazidi kupanda na kutishia maisha ya wananchi hali inayoonekana baadhi ya viongozi waliopewa dhamana kushindwa kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia zaidi muhali kutokana na wanaofanya vitendo hivyo wakiwa na ukaribu nao.

"Visiwa vilikuwa na wagonjwa wachache walioambukizwa virusi vya corona, lakini kutokana na baadhi ya viongozi kushindwa kutekeleza dhamana zao, ongezeko la virusi hivyo linazidi," alisema.

Alieleza kuwa tabia ya dharau na kebehi inayofanywa na baadhi ya watu kutojali kuchukuwa tahadhari dhidi ya virusi vya corona inaweza kuliangamiza taifa katika kipindi kifupi.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar, Makame Khatibu Makame, alisema baadhi ya vyombo vya usafiri wa baharini havijazingatia umuhimu wa kuwa na vifaa vya maafa sambamba na vya kujilinda na maambukizi ya virusi vya corona.

Alisema hali hiyo inaweza kwa kiasi kikubwa kuambukiza kwa haraka virusi hivyo kutokana na msongamano wa abiria katika vyombo hivyo licha ya kuonywa kuchukuwa idadi inayokubalika kwa mujibu wa usajili wa chombo husika. Wakichangia katika kikao hicho, baadhi ya viongozi na watendaji wa taasisi zilizo katika wilaya ya Kaskazini 'A' walieleza changamoto kubwa inayowakabili ni ukosefu wa vifaa vya kutekeleza majukumu yao ya kila siku hasa kipindi hichi cha mlipuko wa janga la virusi vya corona.

Walisema ukosefu wa boti za doria pamoja na magari za kufuatilia matukio pale yanaporipotiwa hasa kipindi hiki cha uingiaji wa watu kutoka nje ya Zanzibar ni changamoto kubwa inayopaswa kuchukuliwa hatua za dharura na Serikali pamoja na taasisi zake ili kupunguza changamoto hizo.

# Kiwanda cha mwani kujengwa Pemba

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema, inakusudia kujenga kiwanda cha kusarifu mwani na kuongeza thamani ya zao hilo huko Chamanangwe kisiwani Pemba katika mwaka wa fedha 2020-2021.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Biashara na Viwanda, Balozi Amina Salum Ali, wakati akitoa ufafanuzi na kujibu hoja za Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wa kamati ya Fedha Biashara na Kilimo ya mwaka 2019-2020.

Balozi Amina alisema hizo ni sehemu za juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Zanzibar katika kuona kilimo cha mwani kinakuwa mkombozi kwa wananchi wa Unguja na Pemba.

Alizitaja juhudi hizo ni pamoja na kuwawezesha wakulima wa kilimo cha mwani kupiga hatua kubwa ya maendeleo na uchumi pamoja na kutafuta soko la uhakika nje ya nchi.

Alisema mafanikio yameanza kuonekana kwa wakulima wa mwani kwa kupanda kwa bei ya zao hilo kutoka Sh.400 hadi kufikiya Sh.1,800 kwa kilo moja.

"Napenda kuwajulisha wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kwamba mikakati ya Serikali kwa sasa ni kuimarisha kilimo cha zao la mwani ambayo hulimwa na wanawake wengi katika mwambao wa pwani ikiwamo kujenga kiwanda cha kusarifu mwani huko Chamanangwe Pemba," alisema.

Aidha, alisema Serikali itaendelea kuweka mipango madhubuti ili kukifanya kilimo cha mwani kuwa cha manufaa ya kibiashara na kubadilisha maisha ya wananchi wanaoishi pembezoni wa mwambao wa pwani.

"Hiyo ndiyo mikakati yetu, kuona kilimo cha mwani kinakuwa cha kibiashara na kunyanyua kipato cha mwananchi wa kawaida wa kijijini ikiwamo wanawake," alisema.

Baadhi ya Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi wamelitaka Shirika la Taifa la Biashara (ZSTC) kujikita katika kununua mwani kama inavyofanya kwa mazao ya viungo ikiwamo karafuu na pilipili hoho ili kuwanyanyua wakulima hao.

Zanzibar ni miongoni mwa nchi tatu katika Bara la Afrika zinazozalisha na kusafirisha zao la mwani kwa wingi duniani katika nchi za Asia na Marekani.

# Mfumo wa kudhibiti mchanga wakaribia

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Zanzibar imesema, inakusudia kuweka mfumo mzuri wa udhibiti wa matumizi ya maliasili zisizorejesheka ikiwamo mchanga baada ya kubaini kuwapo kwa matumizi mabaya.

Akiwasilisha ripoti ya utekelezaji wa maagizo ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2019-2020, Waziri wa Kilimo, Maliasili na Uvuvi, Mmanga Mjengo Mjawiri, alisema kuwapo kwa udhibiti wa mchanga kwa kiasi kikubwa kumewezesha kuwapo kwa bei nafuu na upatikanaji wa mchanga kwa wananchi.

Alisema Serikali pia imeweka mikakati ya udhibiti katika rasilimali ya uchimbaji wa kifusi mawe na kokoto Unguja na Pemba.

Alieleza kuwa awali hakukuwa na udhibiti wa rasilimali hiyo, hivyo kuwafanya baadhi ya watu kujimilikisha machimbo ya mawe na kifusi na kuvuna rasilimali hiyo kiholela.

"Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi imefanikiwa kuweka udhibiti bora wa matumizi ya rasilimali zote ambazo zipo katika hatari ya kutoweka kutokana na kasi ya matumizi yake ikiwamo mchanga, kifusi, mawe pamoja na Kokoto," alisema.

Alieleza kuwa Wizara imefanikiwa kudhibiti rasilimali ya mali zisizorejesheka ikiwamo mchanga kutoka Sh. 558,000,000 mwaka 2015 hadi Sh. 16,549,056 kufikia Februari 2020.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi, Dk. Mwinyihaji Makame Mwadini, aliitaka serikali kuruhusu wafanyabiashara wakubwa ikiwamo kampuni za ujenzi kuingiza mchanga kutoka nje ya nchi ili kukabiliana na uhaba wa mchanga nchini.

Dk. Makame alisema Zanzibar inakabiliwa na uhaba wa rasilimali ya mchanga ambao hautoshelezi mahitaji na matumizi ya ndani.

Alieleza uhaba wa mchanga athari zake zimejitokeza ikiwamo baadhi ya miradi mikubwa ya ujenzi kuchelewa kuanza utekelezaji wake na kumalizika kwa wakati.

TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## ELIMU/ MASOMO

**REGISTRATION OPPORTUNITIES**

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** located at salasala announces registration opportunities for Nursery and Primary School students. Call: 0713 327613.

## NYUMBA/VIWANJA

**NYUMBA INAUZWA,** Ninauza nyumba ya vyumba vinne vya kulala, kimoja ni master self contained. Ina vyumba vitano vya nyuma kimoja ni self contained, choo, bafu na jiko. Nyumba iko Ntyuka Dodoma karibu na shule ya sekondari Ntyuka. Nyumba iko kwenye kiwanja cha ukubwa wa SQM 2590. Ni nyumba nzuri sana kwa makazi na kupangisha. Kwa maelezo zaidi piga simu no. 0699-210258


NIPASHE NI JIBU LAKO

NJOO UTANGAZE NASI

KWA BEI NAFUU SANA

Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu:


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo:**
**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;94/2020**

Ombi la **EMMANUEL WAZIRI KILUSUNGU** Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu **VUMILIA SALEHE MDENG'O.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 20/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/04/2020.

HAKIMU

157039

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NA 27 YA 2020**
**TUJIJENGE TANZANIA LTD……………..MDAI**
**DHIDI YA**
**MARCELA JEREMIAH……………….MDAIWA**
**Kwa, MARCELA JEREMIAH**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya tarehe 27 Mwezi 04 mwaka 2020 saa 2:00 asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusoma hukumu ya shauri hilo ni lazima ufike bila kukosa.

ANGALIZO: Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu bila ya uwepo wako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 14 Mwezi 04 Mwaka 2020.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

157036

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA WILAYA**
**KINONDONI**
**SHAURI LA MADAI NA 28 YA 2020**
**TUJIJENGE TANZANIA LTD……………..MDAI**
**DHIDI YA**
**BEATRICE SALAKANA……………….MDAIWA**
**Kwa, BEATRICE SALAKANA**

**KUITWA SHAURINI**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake ambayo maelezo yake yameelezwa katika nakala za madai ambazo zinaweza kupatikana katika Mahakama hii, kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria katika Mahakama hii binafsi au Wakili au Mwakilishi ambaye anaruhusiwa siku ya tarehe 27 Mwezi 04 mwaka 2020 saa 2:00 asubuhi. Kwa mujibu wa madai hayo, na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusoma hukumu ya shauri hilo ni lazima ufike bila kukosa.

ANGALIZO: Kama hutahudhuria siku iliyotajwa hapo juu na Mahakama ikithibitisha kama umepokea wito wa kuitwa shaurini itaweza kutoa hukumu bila ya uwepo wako.

Hati hii imetolewa kwa amri yangu na chapa ya Mahakama hii leo tarehe 14 Mwezi 04 Mwaka 2020.

HAKIMU MKAZI MFAWIDHI
MAHAKAMA YA WILAYA
KINONDONI

157036

---

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**
**SHAURI No. 98/2019.**
**YOLAM CHANDO.......................MDAI**
**DHIDI YA**
**TANU B.KIYOMBO .......................MDAIWA WA KWANZA**

YAH: KUITWA SHAURINI
KWA: TANU V.KIYOMBO

Fahamu kwamba Yolam Chando amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

shauri limepangwa kutajwa tarehe 16/04/2020 saa 2:30 asubuhi mbele ya Mh; T Munzerere Mwenyekiti katika Baraza unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu.

Nyaraka zinahusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi anayeruhusiwa kisheria. Ofisi za baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya Mjini.

Kumbuka: Usipo hudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.

Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na likiri/muhuri wa baraza hili leo tarehe 16/03/2020.

-----------------------------------------------------------

157030

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5**
**KANUNI YA 2 Katika mahakama ya mwanzo**
**MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;6/4/2020**

Ombi la OSCAR JOHN KITAMBI Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu BERNADETA JOHN GAMBISHI.

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 05/05/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 06/04/2020.

157032

---

**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

ADAM ABDALLAH MALIMA

anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili T 853 ANL TOYOTA CHASER. Chassis namba JZX1006022725. Engine namba JAA002718.

Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi.

Taarifa ya polisi: DOD/DOD/RB/308424/2020.

157031

---

**TANGAZO LA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI**

SAMWEL ZEPHANIA AKYOO ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA YA USAJILI MC 984AHF ENGINE NO 162FMJD5165747 CHASSIS NO LFSGE2PK001643

KWA ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI ARU/ARU/RB/456158/2019.

157033

---

**TANGAZO LA KUPOTEA KWA KADI ZA GARI.**

MARTIN AMANI IYEWE ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI ZA GARI AINA YA NISAN SAFARI YENYE NO YA USAJILI T247CD 241 NA MARCEDES BENZ T247 CD266

KWA YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA POLISI ARU/KIK/RB/309091.

157034

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA WILAYA**
**KAGERA LILILOPO BUKOBA**
**MAOMBI 130/2018**

**LENA JOEL RWEHABURA ...................MDAI**
**DHIDI YA**
**1. NMB BUKOBA BRANCH**
**2. L. J. INTERNATIONAL LTD ....................WADAIWA**
**3. JUSTUS NDIBALEMA**
**4. ERICK GWAJE**

**KWA JUSTUS NDIBALEMA NA ERICK GWAJE**
**(POPOTE PALE WALIPO)**

Mnaarifiwa/unaarifiwa kuwa maombi Na. 130/2018 yamepangwa kutajwa tarehe 30/04/2020 mbele ya mwenyekiti wa Baraza R. Mtei saa 2:00 asubuhi.

Hivyo, unaamuriwa kuhudhuria wewe mwenyewe / mwakilishi wako mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa. Usipohudhuria Baraza litasikiliza shauri upande mmoja dhidi yako na hukumu kutolewa.

AMRI hii imetolewa kwa mkono wangu na muhuri wa Baraza hili leo tarehe 08/04/2020.

BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA
BUKOBA

157043

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**
**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**

Katika mahakama ya Mwanzo
CHAMWINO MJINI
Usimamizi wa Mirathi No. 28/2020.

Ombi la MOSHI HASSAN DARUWESHI kuteuliwa kuwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu DARUWESHI HASSAN NYAGANI

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe23/04/2020 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
TARAHE 14/4/2020.

157042

---

**MAHAKAMA KUU YA TANZANIA**
**KANDA YA MWANZA**
**SHAURI LA MADAI YA UTEKELEZAJI N0 36/2019**
**PHILIMON MWOGOSI……………………MDAI**
**DHIDI YA**
**BURURE MARWA KYARO………………MDAIWA**

**KWA:**
**BURURE MARWA KYARO**
**POPOTE ULIPO**

**KUITWA SHAURINI**

Unaarifiwa wewe au wakili wako kuhudhuria hapa mahakamani bila kukosa tarehe 22/4/2020, kuja kusikiliza shauri la madai lililofunguliwa dhidi yako.

Unatahadharishwa kuwa endapo hautofika siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja dhidi yako na kutolewa maamuzi.

Hati hii imetolewa kwa mkono wangu na chapa ya mahakama leo hii tarehe 30/3/2020.

NAIBU MSAJILI
MAHAKAMA KUU YA TANZANIA
MWANZA

157044

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo**

**MJINI-MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;96/2020**

**Ombi la FORTUNATHA PAULO MSAWANGA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu SIGHSBERT RAJABU MBARUKU**

**Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 24/04/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.**

**Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 06/04/2020.**

HAKIMU

157041

---

**KUPOTEA KWA KADI YA KADI**

GEORGE NGUGI KAMAU

Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba ya usajili T521AAV BMW, Rangi Metalic Engine No.06869376 Chassis No. WBAA920NBA10965 Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

Taarifa ya polisi ARU/ARU/RB/313812/2020

157047


Uza, Chenye Thamani Kubwa

Kwa Kutangaza Nasi

Kwa Bei Poa

Tupigie 0782253676



OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 745 700 710.
E-mail: advertise@guardian.co.tz, website: www.ippmedia.com



TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

## HABARI KIMATAIFA

# Ukikutwa hujavaa barakoa faini elfu 20

**NAIROBI,** Kenya

JESHI la Polisi nchini Kenya, limeanza rasmi kukagua utekelezaji wa amri ya kuvaa barakoa mitaani kama njia ya kuzuia kusambaa kwa virusi vya corona.

Limesema atakayepatikana bila barakoa mtaani atatozwa faini ya Sh. 20,000 au kufungwa kwa muda usiozidi miezi sita au vyote.

**Lakini Wakenya wamekuwa wakiitaka serikali kuwapa barakoa bure.**

Mkuu wa Jeshi hilo, Hillary Mutyambai, alisema kuwa Wakenya wameshapewa muda wa kutosha kujipatia vazi hilo la kujikinga.

Mwishoni mwa wiki iliyopita, Waziri wa Afya wa Kenya, Mutahi Kagwe, aliwasilisha kwenye gazeti rasmi la serikali adhabu ambazo zinaweza kutolewa kwa watakaokiuka sheria hiyo.

Kagwe aliwataka wafanyakazi wa biashara ya maduka ya jumla, saluni na kusuka nywele, sharti wavae barakoa wanapowahudumia wateja.

Hata hivyo, suala la ubora wa barakoa hizo linazua utata. Baadhi ya barakoa zinashonwa mitaani pasina kujali kanuni za usafi wala afya.

Kwa upande wake Waziri wa Biashara na Viwanda, Betty Maina, alibainisha wiki iliyopita kuwa, kampuni za kutengeneza nguo za Kenya zina malighafi ya kutosha kushona barakoa milioni sita.

Viwanda vya Kicotex vilivyopo Kitui na Rivatex ya Eldoret ndivyo vilivyopewa wajibu wa kushona barakoa zitakazotimiza vigezo vya afya na kuwa bei nafuu.

Lakini Wakenya wamekuwa wakiitaka serikali kuwapa barakoa bure.

Kulingana na Shirika la Afya Ulimwenguni (WHO), barakoa zinapunguza uwezekano wa kusambaza mate na majimaji yenye virusi vya corona endapo mtu anapokohoa au kuzungumza. **DW**




Maofisa wa polisi nchini China, wakiwa mtaani wakipulizia dawa ili kudhibiti maambuzi ya ugonjwa wa virusi vya corona. **PICHA: REUTERS**

## Watishia kutoroka karantini, wagonjwa wakiongezeka

**NAIROBI,** Kenya

IDADI ya watu waliokuwa katika karantini ya lazima nchini Kenya, wamefanya mgomo na kutishia kutoroka katika kituo hicho katika mji mkuu wa Nairobi.

Wanadai kwamba kusalia kwao katika vituo hivyo sio haki kwa kuwa wamepimwa mara mbili na kukosekana kuwa na virusi hivyo.

Wiki iliyopita, serikali ilitangaza kwamba muda wao wa kusalia karantini utaongezwa kutoka wiki mbili hadi mwezi mmoja baada ya kubainika wakikaidi baadhi ya maagizo ya serikali kukabiliana na virusi vya corona.

Lakini baadhi ya wale walio katika karantini wanasema kwamba wanaugua shinikizo la kiakili.

Kundi hilo la watu 21 ambalo limekuwa likiishi katika chuo kikuu cha Kenya (KU) liliagizwa kusalia baada ya vipimo vya hivi karibuni kuwapata wawili wao na virusi .

Hatua hiyo inajiri huku Kenya ikiripoti wagonjwa wengine tisa wa virusi vya corona na kufanya idadi ya waliopatikana na ugonjwa huo kufikia 225. **BBC**

# Congo yapambana na ebola, corona

**KINSHASA,** Congo

JAMHURI ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), kwa sasa inapambana na magonjwa mawili ya mlipuko ambayo ni ebola na corona.

Wakati maambukizi ya kwanza ya ugonjwa wa virusi vya corona yalipothibitishwa nchini humo Machi, taifa hilo lilikuwa limetangaza kuwa liko huru na ugonjwa wa ebola kwa wiki kadhaa.

Ilidhaniwa kuwa, vifaa tiba ambavyo vilitumika kukabiliana na ugonjwa huo vingeweza kukabiliana na ugonjwa wa virusi vya corona.

Lakini Ijumaa, ikiwa ni siku mbili tu baada ya Shirika la Afya Duniani (WHO) kutangaza mwisho wa mlipuko wa ugonjwa wa ebola uliosababisha vifo zaidi ya 2,000, wagonjwa wengine waliripotiwa kupata maambukizi ya ebola mjini Beni mashariki mwa nchi hiyo.

Wakati ugonjwa wa corona ukisambaa nchini humo, mamlaka ya afya sasa imeanza kukabiliana na magonjwa hayo mawili hatari.

Maambukizi ya ugonjwa wa ebola yalisambaa zaidi Mashariki mwa congo tofauti na corona ambayo imesambaa katika mji mkuu wa Kinshasa hadi kwenye majimbo yenye mgogoro ambapo kuna wagonjwa 235 walioripotiwa.

Dunia sasa inakabiliana na janga hilo la kutafuta tiba au chanjo pamoja na msaada wa kuweza kukabiliana na ugonjwa wa mlipuko.

Mchanganyiko wa taarifa kuhusu magonjwa yanayoambukiza barani Afrika, yameondoa imani ya watu kwa serikali zao kuwa na uwezo wa kukabiliana na magonjwa ya mlipuko.

Alisema kuwa ugonjwa huo ni sawa na timu mbili tofauti.

Alisema kutokomezwa kwa ugonjwa wa ebola kulileta matumaini kuwa baadhi ya rasilimali ambazo zilitumika kwa kipindi cha miezi 20 kuwatibu wagonjwa wa ebola, ikiwa ni pamoja na maabara, vifaa tiba na wataalamu wa afya ambao walielimishwa jinsi ya kukabiliana na magonjwa yanayoambukiza.

Maambukizi ya ebola kwa mwanamume mwenye miaka 26, yamesababisha utafiti kufanyika ili kubaini wapi aliambukizwa. **BBC**

## Marekani kusitisha ufadhili WHO

**WASHINGTON,** Marekani

RAIS wa Marekani, Donald Trump, amesema kuwa uongozi wake utasitisha ufadhili kwa Shirika la Afya Duniani (WHO).

Amesema WHO imeshindwa kufanya majukumu yake muhimu katika kukabiliana na mlipuko wa virusi vya corona.

Vilevile ameishutumu Umoja wa Mataifa (UN) kwa kutoweza kukabiliana na kusambaa kwa ugonjwa huo ambao ulianzia nchini China, na linapaswa kulaumiwa.

Rais Trump awali aliishutumu WHO kwa kuipendelea China.

Aidha, Rais Trump mwenyewe alikosolewa kwa namna anavyokabiliana na mlipuko huo nchini mwake.

"Ninawapa muongozo, utawala wangu kusitisha ufadhili wakati Shirika la Afya duniani likiwa linachunguzwa katika majukumu yake yaliyoshindwa kuyatimiza katika kukabiliana na usambaaji wa virusi vya corona ," alisema Trump wakati akizungumza na waandishi wa habari Ikulu.

Rais Trump alisema WHO limeshindwa majukumu yake muhimu na wanapaswa kuwajibishwa.

HABARI MICHEZO




# POGBA: NILIKUWA SHABIKI WA ARSENAL

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa Manchester United, Paul Pogba, amebainisha kuwa wakati anakuwa alikuwa shabiki wa Arsenal kwa sababu ya Thierry Henry ambaye ni raia mwenzake wa Ufaransa.

Pogba yupo kwenye kipindi cha pili pale United, awali alijiunga na mashetani wekundu hao wakati akiwa na umri wa miaka 16 akitokea Le Havre mwaka 2009 kabla ya kwenda Juventus miaka mitatu baadae na kurudi kwa ada iliyoweka rekodi mwaka 2016.

Lakini Pogba awali alionyesha mahaba yake kwa Arsenal, akiiambia tovuti ya United: "Nitakuwa mkweli. Mwanzo nilikuwa shabiki wa Arsenal, na hasa kwa sababu ya wachezaji wa Ufaransa, kama unavyojua.

"Mimi na kaka yangu tulikuwa mashabiki wa Arsenal, lakini kaka yangu mwingine ilikuwa shabiki wa Manchester United.

"Nilikuwa nampenda Henry na kwa sababu ya yeye ndio nilikuwa shabiki wa Arsenal. Halafu nikabadilika na kaka yangu. Nikaachana na Arsenal, nikaenda klabu nyingine, shabiki wa United!"

# Herrera asifia mchango wa Neymar

**PARIS,** Ufaransa

KIUNGO wa Paris Saint-Germain, Ander Herrera, amesifia mchango wa "ajabu" wa Neymar kwa klabu hiyo ya Ligi Kuu Ufaransa, Ligue 1.

PSG walikuwa kileleni mwa msimamo wa Ligue 1 na wapo kwenye robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Ulaya pamoja na Kombe la Ufaransa – wakati msimu uliposimamishwa kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

Herrera amezungumzia jitihada za mchezaji huyo wa Brazil, Neymar kwa PSG, hasa kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya hatua ya 16 dhidi ya Borussia Dortmund.

"Wote tulikwenda nyumbani kwake kula chakula pamoja... alikuwa ni mtu mwenye hamasa. Alipambana kwa hali na mali," alisema akiiambia Canal+ Jumanne.

"Wakati nilipowaona waandishi wachache wanasema Neymar alikuwa haifikiri PSG, nilishangaa, kwani mchango wake kwa timu ulikuwa ni wa ajabu.

"Neymar alijitoa kwa hali na mali kwa timu. Mchezaji wa daraja A ambaye anajitoa kwa timu kama yeye inamaana kubwa na huifanya timu kuwa na umoja."

Herrera pia ana matumaini msimu wa Ligi Kuu utarudi na kuendelea tena licha ya kusimama kutokana na virusi vya corona.







# *Wakala hana hofu hatima ya Van de Beek*

**AMSTERDAM,** Uholanzi

WAKALA wa Donny van de Beek, amesisitiza hakuwa na hofu kuhusu majaliwa ya baadaye ya kiungo huyo wa Ajax.

Van de Beek amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kutoka kwa miamba hao wa Ligi Kuu Uholanzi, Eredivisie, huku Real Madrid na Manchester United zikiripotiwa kumwania.

Wakala wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22, Guido Albers, amesema huku soko la usajili linaweza kuwa tofauti kutokana na corona, majaliwa ya Van de Beek bado sio jambo la kulijadili sana.

"Itakuwa tofauti, lakini lazima niwe mkweli," alisema akiiambia televisheni ya Voetbal International.

"Pia inatengeneza nafasi kwa klabu nyingine kugonga mlango licha ya kwamba hazikuwa na mpango nae.

"Sina hofu kuhusu Donny."

Albers hakuwa tayari kuzungumzia kwa undani kuhusu klabu ambazo zinamwania Van de Beek, lakini amesema bado kuna ofa nyingi zinakuja.

# Man United kumng'oa Niguez Atletico

**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United inaangalia uwezekano wa kumsajili kiungo wa Atletico Madrid, Saul Niguez huku wakimpa ofa ya mshahara wa pauni 85,000 kwa wiki zaidi ya anaolipwa sasa.

Miamba hao wa Ligi Kuu England kwa muda mrefu wamekuwa wakimfuatilia mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 25 lakini kwenye mkataba wake ana kipengele cha kuondoka kwa pauni milioni 135.

United itajaribu kumwongezea mshahara wake wa wiki kutoka pauni 115,000 hadi pauni 200,000 kwa wiki, kwa mujibu wa gazeti la The Sun.

Klabu hiyo ya Old Trafford imeripotiwa kwamba imeandaa kutoa ofa ya pauni milioni 70 kama ada ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Hispania. United ilituma maskauti wake kumwangalia Saul wakati akiisaidia kuitupa nje Liverpool kwenye Ligi ya Mabingwa Ulaya mwezi uliopita.

Anaonekana kuwa atafiti kwenye kikosi cha United chini ya Ole Gunnar Solskjaer ambaye anaendelea kukijenga kikosi chake. Saul alisaini mkataba wa muda mrefu pale Atletico mwaka 2017 ambao unamalizika mwaka 2026.

Saul amefunga mabao manne katika mechi 37 za Atletico msimu huu, likiwamo goli la ugenini kwenye mchezo wa kwanza hatua ya mtoano wa 16 dhidi ya Liverpool mjini Madrid.



# AC MILAN YASHAURIWA KUMSAJILI ICARDI



**MILAN,** Italia

AC Milan inatakiwa kumsajili, Mauro Icardi kutoka kwa wapinzani wao Inter Milan ili kuifanya safu yao ya ushambuliaji kuwa bora zaidi, kwa mujibu wa Marco Simone.

Antonio Conte alimwondoa Icardi katika mipango yake wakati Inter ikijiandaa na msimu wa 2019-20, na badala yake wakamchukua Romelu Lukaku kuwa patina wa Lautaro Martinez.

Icardi alipelekwa kwa mkopo Paris Saint-Germain, ambapo alimweka benchi mfungaji wa wakati wote wa kabu hiyo, Edinson Cavani katika kikosi cha kwanza akifunga mabao 20 katika mechi 31.

Simone anaamini Milan wanahitaji kuimarisha safu yao ya ushambuliaji na anafikiri Cavani au nahodha wa zamani wa Inter, Icardi mmoja wao anaweza kuwa suluhisho la matatizo yao kama mkataba wa Zlatan Ibrahimovic hautaongezwa mwishoni mwa msimu huu.

Rossoneri hao wanashika nafasi ya saba kwenye msimamo wa Ligi Kuu Italia, Serie A, huku ikiwa imefunga mabao machache zaidi kabla ya ligi hiyo kusimama kutokana na mlipuko wa virusi vya corona.

"Ningemchukua Icardi au Cavani ili kuimarisha safu ya ushambuliaji kwani ni wachezaji wenye vipaji vya ukweli," amesema Simone, ambaye alishinda mara nne Kombe la Ligi Kuu Italia na mataji mawili ya Ligi ya Mabingwa Ulaya akiwa na Milan, akiiambia gazeti la La Gazzetta dello Sport.

Milan ilimfukuza ofisa wake wa soka, Zvonimir Boban, baada ya kuzungumza hadharani kutofurahishwa na mbinu za Ofisa Mtendaji Mkuu Ivan Gazidis.

# Aguero ahifadhiwa jezi na. 10

**BUENOS AIRES,** Argentina

JEZI namba 10 inayopendwa na Sergio Aguero, imehifadhiwa kwa ajili yake na klabu ya Independiente, amesema kocha Lucas Pusineri.

Mfungaji huyo wa wakati wote pale Manchester City, aliondoka katika klabu yake hiyo ya utotoni na kujiunga na Atletico Madrid miaka 14 iliyopita na mara kwa mara amekuwa akizungumzia mpango wake wa kwenda kumalizia soka lake pale Independiente maarufu kama El Rojo.

Aguero mwenye umri wa miaka 32 mkataba wake wa sasa na City unamalizika mwaka 2021, na kuteuliwa kwa mchezaji mwenzake wa zamani, Pusineri kuwa kocha wa Independiente mapema mwaka huu kumeongeza ushawishi wa mchezaji huyo kurudi nyumbani.

"Matumaini yangu nitakuwa kocha wa Kun Aguero," alisema Pusineri akiliambia gazeti la Super Miter Deportivo.

"Alikuwa mchezaji mwenzangu na matumaini yangu siku zijazo atarudi na kuendelea kucheza hapa chini yangu. "Natumaini kukaa kwangu hapa Independiente, naweza kuungana na yeye Sergio. Tumeihifadhi jezi namba 10 kwa ajili yake."

Pusineri alibainisha pia kuwa kuna mawasiliano ya mara kwa mara na nyota huyo wa kimataifa wa Argentina, ingawa alikanusha madai ya kumshawishi kurudi pale Independiente.

Aguero amefunga mabao 254 katika mechi 368 pale City, huku 180 yakiwa kwenye Ligi Kuu na kumfanya ashike nafasi ya nne kwenye orodha ya wafungaji wa wakati wote wa Ligi Kuu England, ambapo pia amefunga 12.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# ARSENAL YAJIPANGA KUMNUNUA PARTEY

●●● Yawasilisha dau nono ili kumnasa kiungo huyo Mghana anayeichezea Atletico...

**LONDON,** England

HAITAKI mchezo! Hii ni kauli ambayo unaweza kusema inatoka kwa mabosi wa Arsenal baada ya kuweka mezani dau la pauni milioni 43.5 kwa ajili ya kuwania saini ya nyota wa Atletico Madrid, Thomas Partey, imefahamika.

**Kiungo huyo raia wa Ghana amekuwa mmoja wa wachezaji muhimu katika kikosi cha Wanda Metropolitano msimu huu, akicheza mechi 35 za mashindano mbalimbali na kuisaidia Atletico Madrid kutinga hatua ya robo fainali ya michuano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya.**

Hata hivyo, licha ya mkataba wa Partey kuonyesha kiasi anachotakiwa kuuzwa endapo kuna klabu nyingine itamhitaji, gazeti la Corriere dello Sport, limeandika Mikel Arteta imewasilisha rasmi dau la pauni milioni 43.5 kama ofa yake.

Taarifa katika gazeti hilo maarufu la michezo zimeandika kuwa nyota huyo tayari ameshaanza kujiandaa kujiunga na klabu hiyo inayotumia Uwanja wa Emirates.

Tangu alipojiunga na Arsenal hapo Desemba mwaka jana, Arteta amekuwa akipambana kukijenga kikosi hicho ili msimu ujao awe na timu iliyoimarika baada ya kuwa na msimu wenye matokeo mabaya.

The Gunners iko katika nafasi ya tisa kwenye msimamo wa Ligi Kuu England, ikiwa imeshinda mechi tisa kati ya michezo 28 iliyotarajiwa, na Arteta amekuwa akiongeza nguvu ili kuirejesha timu hiyo kwenye ubora wake na ndani ya 'Top Four.'

Arteta anatajwa amekuwa na mpango wa kuimarisha safu yake ya kiungo wakabaji kutokana na kuyumba kwa wachezaji waliokuwapo na kutoa nafasi ya safu ya ulinzi kupata msaada, wakati Lucas Torreira na wenzake wakiendelea kupambana kuwania namba katika kikosi cha kwanza.

Licha ya mkataba wa Partey kubakiza miaka mitatu, Atletico tayari ilikuwa imeshaanza mchakato wa kumpatia mkataba mpya wa kuendelea kuitumikia klabu hiyo.

Vigogo hao wa LaLiga wanataka kuona nyota huyo ambaye yuko katika kiwango cha juu sasa, akipandishiwa mshahara wake na wanaamini hiyo itasaidia kumfanya abakie kwenye timu yao hadi mwaka 2025 huku ikimpatia mshahara mnono.

## ZISIKUPITE

### INTER WAITEGA BARCA

INTER Milan imesema itahitaji kupewa mshambuliaji Mfaransa Antoine Griezmann (29), ili kumtoa straika Lautaro Martinez kama Barcelona inataka kumsajili nyota huyo raia wa Argentina mwenye umri wa miaka 22. ***(La Gazzetta dello Sport, via Marca)***

### BARCA YAMTAJA ISAK

MABOSI wa Barcelona wamesema watafanya mchakato wa kumsajili mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Sweden, Alexander Isak, ambaye ana umri wa miaka 20, akitokea Real Sociedad kama watashindwa kunasa saini ya Martinez. ***(Marca)***

### KANTE ANUKIA MADRID

KIUNGO wa Chelsea na Timu ya Taifa ya Ufaransa, ielder N'Golo Kante (29), ni mmoja kati ya nyota watatu wanaowindwa na Real Madrid katika dirisha lijalo la usajili.***(AS, via Mail)***

### KANE APELEKWA BARCA

KOCHA wa zamani wa Tottenham, Harry Redknapp, amesema straika Harry Kane hataweza kuendeleza kipaji chake kwa kujiunga na Manchester United lakini nahodha huyo wa England ataimarika endapo ataelekea Barcelona au Real Madrid. ***(Talksport)***

### COUTINHO ANUKIA EPL

ARSENAL na Chelsea zitakuwa katika nafasi nzuri ya kumsajili kiungo mchezeshaji wa Barcelona, Philippe Coutinho (27), kwenye majira ya joto kufuatia Bayern Munich kusitisha mpango wa kumpa mkataba wa kudumu Mbrazil huyo ambaye alikuwa akiitumia klabu hiyo kwa mkopo. ***(Sun)***

### UNITED YAMGANDA NIGUEZ

MANCHESTER United inaendelea kumfuatilia kiungo wa Atletico Madrid, Saul Niguez, lakini kwa kulipa ada ya pauni milioni 70 badala ya pauni milioni 132 ambazo zimewekwa katika mkataba wake. United inajipanga kumlipa Mhispania huyo mshahara wa pauni 115,000 kwa wiki na utaongezeka hadi kukaribia pauni 200,000 kwa wiki hapo baadaye. ***(Sun)***

### DE BEEK AGOMBEWA ULAYA

WAKALA wa kiungo wa Ajax, Donny van de Beek (22), amesema nyota huyo anayeichezea Timu ya Taifa ya Uholanzi ambaye anahusishwa na kutakiwa na Real Madrid na Manchester United, anatakiwa na klabu mbalimbali nyingine duniani. ***(Voetbal International, via Metro)***

### HAALAND ATAJWA SOKONI

MANCHESTER United na Real Madrid hazitaweza kuboresha dau la straika wa Borussia Dortmund na Timu ya Taifa ya Norway, Erling Braut Haaland ambao ni pauni milioni 65 katika majira ya joto kwa sababu haiwezi kubadili mwelekeo hadi ifikapo mwaka 2022. ***(Mirror)***

### INSIGNE KUZEEKEA NAPOLI

MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Italia, Lorenzo Insigne, ambaye ana umri wa miaka 28 anajiandaa kusaini mkataba mpya utakaomweka Napoli hadi mwaka 2025. ***(Calciomercato)***

### NEWCASTLE YAPIGWA BEI

MMILIKI wa Newcastle United, Mike Ashley, amesema atakuwa tayari kuiuza klabu hiyo endapo mnunuzi atakayejitokeza atatoa kiasi cha pauni milioni 300. ***(Mail)***

## HABARI MICHEZO

## Coastal Union kusajili baadaye

**Na Shufaa Lyimo**

UONGOZI wa Coastal Union yenye maskani yake jijini Tanga, umesema kwa sasa hautasajili mchezaji yoyote mpaka hapo dirisha la usajili litakapofunguliwa rasmi na Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), imefahamika.

Mwenyekiti wa Coastal Union, Steven Mguto, alisema klabu hiyo haitafanya mazungumzo na mchezaji yeyote kwa sasa na badala yake itaendelea kusimamia mazoezi ya timu kwa ajili ya kumalizia mechi zilizosalia kama Ligi Kuu Bara itaendelea tena.

Mguto alisema Coastal Union imeamua kusimamisha shughuli zote za kiutendaji mpaka pale janga la maambukizi ya virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19) litakapomalizika.

"Kwa sasa hatuna muda wa kuzungumzia usajili mpaka hapo janga hili la corona litakapomalizika, kwa kiasi kikubwa Watanzania tuungane kwa pamoja kuomba ugonjwa huu upungue ili tuweze kuendelea na majukumu mengine," alisema Mguto.

Aliongeza kwa sasa wanachokifanya ni kuhakikisha kila mchezaji anafanya mazoezi ya binafsi kwa kufuata maelekezo waliyopewa na kocha wao, Juma Mgunda, ili kuiweka sawa miili yao wakati wakisubiri uamuzi mpya utakaotolewa na TFF baada ya kufuata mwongozo wa serikali.

"Tunaomba kila mchezaji awe makini kwa kufuata maelekezo aliyopewa na mwalimu ili kujiweka sawa, hii itawasaidia kulinda viwango vyao katika kipindi hiki ambacho hakuna mechi zozote," Mguto alisema.

## Sputanza yaita wachezaji Bara

**Na Mwandishi Wetu**

NYOTA wanaoshiriki Ligi Kuu Bara wametakiwa kujiunga na Chama cha Wachezaji wa Soka Tanzania (Sputanza), kwa lengo la kuwaongoza katika mambo mbalimbali na kamwe kutosubiri kufikwa na matatizo.

Wito huo pia unawahusu wachezaji wa timu za Ligi Daraja la Kwanza, Ligi Daraja la Pili na Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania. Katibu Mkuu wa Sputanza, Said George, aliliambia gazeti hili jijini Dar es Salaam jana kuwa, chama hicho kimeundwa kwa lengo la kuwasaidia na kuwaunganisha wachezaji wote wa mpira wa miguu.

Said alisema wanawakumbusha wachezaji kujiunga na umoja huo ambao utasaidia kuwaelimisha kufanya uamuzi wa mambo mbalimbali ambayo yatawasaidia katika maisha yao ya kila siku.

"Ili kupeusha malumbano na migogoro ya mara kwa mara, tunawakumbusha wachezaji na viongozi wa klabu zote kuheshimu kanuni na taratibu za usajili, kila upande ujue mipaka yake, kikubwa wachezaji wasikae mbali na Sputanza, hiki ni kiunganishi chao," alisema katibu huyo.

Sputanza ni chama shiriki cha Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kama kilivyo Chama cha Waamuzi (FRAT) na Chama cha Soka la Wanawake Nchini (TWFA).

# CHUJI AVUNJA RASMI MKATABA NA SINGIDA

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkongwe nchini, Athumani Idd 'Chuji', amesema amevunja mkataba wake na klabu yake ya Singida United kwa sababu hawakumpa mshahara wa miezi mitatu.

**Akizungumza jijini Dar es Salaam, Chuji alisema kwa sasa si mchezaji wa Singida United kwa sababu wamevunja makubaliano, kwani kwenye kipengele cha mkataba alisaini kuwa asipolipwa mshahara wa miezi miwili basi mkataba wake umevunjika.**

"Kwa sasa niko huru kwa sababu nilisajiliwa kumalizia ligi kipindi cha dirisha dogo, lakini hadi naondoka nilikuwa sijalipwa miezi mitatu," alisema Chuji ambaye ni mmoja wa wachezaji wachache waliowahi kuzichezea klabu kubwa nchini za Simba, Yanga na Azam FC.

Kwa maana hiy,o kiungo huyo mkabaji, aliyekuwa akisifika kwa mashuti makali na pasi ndefu za uhakika, amejiweka sokoni ili timu yoyote inayomtaka ifanye mawasiliano naye.

Kuhusu klabu ya Singida United, Chuji alisema, anayejitahidi kwa sasa kuhakikisha haishuki na kuendelea kucheza ligi ni Waziri wa zamani wa Mambo ya Ndani, Mwigulu Nchemba, ambaye anaonekana yupo karibuni na timu, huku baadhi ya viongozi wakionekana kama kuisusa.

"Nashangaa watu wa Singida siyo kama wa Mtwara ambako Ndanda FC kila mwaka inapokuwa kwenye hali mbaya, basi wanakwenda kwa viongozi wa mkoa kama vile Mkuu wa Mkoa na viongozi wengine wa kisiasa kuhamasisha wananchi timu kuwa haishuki na wanafanikiwa sana kwa hilo, Ndanda huwa inasalimika kwa kubakia Ligi Kuu, nashangaa kwa nini watu Singida hawafanyi hivyo." alisema.

Chuji pia aliwalaumu baadhi ya watu ndani ya klabu hiyo kutaka ishuke kwa maslahi yao, halafu waipandishe.

"Mimi nishawasikia kuna watu wanasema wanataka timu ishuke, halafu wao wataipandisha, sasa hawa wanaitakia mema klabu au wana maslahi yao?" alihoji.




Beki wa Timu ya Soka ya Wanawake (Twiga Stars), Fatuma Issa (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya nyota wa Algeria katika mashindano ya Kombe la UNAF yaliyofanyika hivi karibuni nchini Tunisia. Twiga Stars ilishinda mabao 3-2. **PICHA: SOMOE NG'ITU**

# *Corona chanzo ZFF kufunga ofisi*

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

SHIRIKISHO la Soka Zanzibar (ZFF), limefunga ofisi zake kuanzia Aprili 14, mwaka huu, ikiwa njia mojawapo ya kujikinga na virusi vya corona (COVID-19) ambavyo vinaitesa dunia kwa sasa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu Mkuu wa shirikisho hilo, Mohamed Ali Hilali, ilieleza, ZFF itawasiliana na wanachama wao pale inapohitajika huduma kwa njia za simu ya mkononi pamoja na barua pepe ya shirikisho hilo.

Alisema ZFF imechukua uamuzi huo ili kuendelea kushirikiana na serikali katika kujikinga na virusi hivyo hatari ikiwamo kuepuka mikusanyiko katika kipindi hiki kigumu inachopitia dunia.

Aidha, alisema pia wamesitisha mikutano na mahojiano ya moja kwa moja na waandishi wa habari badala yake taarifa zitatolewa kwa njia ya taarifa za maandishi kwa vyombo vya habari mpaka pale serikali kupitia Idara ya Habari Maelezo Zanzibar itakapotoa tamko juu ya mikutano hiyo.

Hata hivyo amewataka wadau wa soka na wachezaji kuendelea kuchukua hatua ya kujikinga na virusi vya Corona kwa kuacha kufanya mazoezi kwa mikusanyiko katika sehemu mbalimbali ikiwamo ufukweni ili kuunga mkono juhudi za serikali kukabiliana na ugonjwa huu hatari.



Arsenal yajipanga kumnunua Partey

UKURASA 22

KUJIFUA...



Viungo wa Simba, Clatous Chama (kushoto), na Muzamiru Yassin, wakifanya mazoezi kujiandaa na mechi za Ligi Kuu msimu huu, kabla haijasimamishwa kutokana na virusi vya ugonjwa wa corona (COVID 19). **PICHA: MAKTABA**

# Mwakalebela mambo magumu

## ●●● Ni baada ya Simba kumshitaki TFF, akikutwa na hatia kuigharimu pia Yanga...

**Na Somoe Ng'itu**

SAKATA linaendelea baada ya Klabu ya Simba kutinga katika Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kwa lengo la kumshitaki Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela kwa tuhuma za kufanya mazungumzo na kiungo wake, Clatous Chama, kinyume na kanuni za usajili zinavyoelekeza, imeelezwa.

**Hata hivyo Mwakalebela ameomba radhi kwa Simba, TFF na Yanga kwa kauli hiyo aliyoitoa na kueleza kwamba alikuwa akiwatania na si kweli amefanya mazungumzo yoyote na kiungo huyo raia wa Zambia.**

Akizungumza na gazeti hili jana, Ofisa Habari na Mawasiliano wa TFF, Clifford Ndimbo, alisema Simba imewasilisha malalamiko katika shirikisho hilo dhidi ya kauli iliyotolewa na Mwakalebela ya kufanya mazungumzo na mchezaji wao ambaye bado ana mkataba na klabu hiyo.

Ndimbo alisema vinara hao wa Ligi Kuu Tanzania Bara wanaomba Mwakalebela achukuliwe hatua kali kwa sababu kitendo alichokifanya ni cha ukiukaji wa kanuni za usajili za TFF na Shirikisho la Soka la Kimataifa (Fifa).

Ofisa huyo wa TFF alisema malalamiko hayo yamepelekwa katika Kamati ya Sheria na Hadhi za Wachezaji ambayo iko chini ya Mwenyekiti wake, Elias Mwanjala.

"Katika malalamiko hayo, Simba imeomba ichukuliwe hatua stahiki ili kulinda kanuni zinazotawala mpira wa miguu pamoja na weledi," alisema Ndimbo.

Mkuu wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Haji Manara, alisema klabu hiyo imeamua kuchukua hatua dhidi ya kiongozi huyo ili iwe fundisho kwa wadau wote ambao wanaenda kinyume na kanuni na taratibu za mpira hapa nchini.

Manara aliweka wazi Chama ambaye ana umri wa miaka 28 ana mkataba na klabu hiyo ambao utamalizika ifikapo Julai mwakani na si miezi sita kama alivyotangaza kiongozi huyo wa zamani wa TFF.

"Inaonekana jambo hili nimelizungumza limevuka mipaka, basi natumia fursa hii kuomba msamaha Simba, TFF na wenzangu wa Yanga. Labda nilizidisha utani, naamini kabisa jambo hili halitaweza kutokea tena kwangu," Mwakalebela alisema.

Endapo Mwakalebela atakutwa na hatia,kwa mujibu wa kanuni ya 70 (5), atatozwa faini au Yanga kuzuiwa kusajili kwa kipindi cha mwaka mmoja hadi mitatu.

# Eymael aipeleka Yanga kimataifa

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa Yanga, Luc Eymael, amesema ana imani hajakosea katika ripoti ya kiufundi ambayo aliiacha kuhusiana na suala la kusajili wachezaji wapya anaowahitaji kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara na mashindano yote watakayoshiriki.

Akizungumza na Nipashe jana, Eymael alisema amejiandaa kukamilisha mchakato huo kwa umakini ili malengo yake ya kujenga kikosi imara yakamilike.

Mbelgiji huyo alisema anataka kuona Yanga inasajili wachezaji watakaoisaidia timu katika mechi zote na si vinginevyo.

"Nilipotua nchini na kukabidhiwa majukumu nimekuta tayari Yanga imeshasajili na kubaki nafasi moja, nilimpendekeza Bernard Morrison, lakini pia niliahidi kwa Wanayanga nikiachiwa jukumu la kusajili basi nitahakikisha ninaleta wachezaji bora zaidi," alisema Eymael.

Kocha huyo alisema mbali na kusajili wachezaji wapya, pia ameutaka uongozi wa klabu hiyo kuhakikisha nyota wa zamani waliomaliza mikataba yao ambao bado anawahitaji kuwapa mikataba mipya ili waendelee kuitumikia Yanga.

Hata hivyo kocha huyo alikataa kuweka wazi majina ya wachezaji ambao amependekeza wabakie katika kikosi hicho kwa sababu ya kuridhishwa na viwango vyao.

Tayari mabosi wa Yanga wameshawapa mikataba mipya Bernard Morrison, Said Makapmu na Papy Tshishimbi yuko katika hatua za mwisho za kukamilisha mazungumzo ya kusaini mkataba mwingine na klabu hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002